# Nipashe

Jumatatu Aprili 1, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581633

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital  nipasheTZ  nipasheTZ  nipasheTZ  0745 700710

LIKE & FOLLOW US


**Mtumbwi** walipuka moto ziwani, wawili wahofiwa kufa maji

UKURASA 7

**Mwaka** mmoja, mimba 196 kwa watoto wilayani

UKURASA 7

**Mwalimu** jela miaka 30 kwa kunajisi mwanafunzi wake

UKURASA 8




UKURASA 11

## MAASKOFU WAONYA

# Jamii iko hatarini

- **Watoa** angalizo kwa Bunge, serikali na mahakama... *Ukurasa 2, 3 & 4*



"Wakikuletea (fedha) wewe pokea tu, weka mfukoni, kula lakini kwenye kura wapige chini. Hapa niwaombe wagombea wanaotumia rushwa kutafuta kura, huo si uzalendo, ni ubinafsi."
**LIBERATUS SANGU**



"Ndio maana ndugu zangu, sisi wakristo tumemaliza mfungo wetu leo, hatuna budi kusherehekea, lakini kwa kuheshimu wenzetu ambao bado wako katika mfungo wao."
**AUGUSTINO SHAO**



"Moyo wangu umesononeka sana kusikia tena Watanzania wengine bado wanaanza kuwindana kwa kutumia risasi kama wanyama."
**ALEX MALASUSA**

"Kama Mwalimu Nyerere alivyosema rushwa ni adui wa haki, tusingependa iendelee kuota mizizi katika maeneo nyeti ya nchi yetu kama vile mahakamani."
**DICKSON CHILONGANI**



"Tusipoangalia maslahi ya walimu na madaktari, ninaiona hatari, sina neno na mishahara ya wabunge. Walipwe hata (shilingi) milioni 20. Sina neno nayo, lakini..."
**FREDRICK SHOO**



"Utaona sasa wavulana wametoga masikio, wamevaa suruali iko chini. Hiyo kwa nchi nyingine ukiona mtu amevaa hivyo, huyo anakuwa ni shoga, mkanye mtoto mapema."
**JOVITUS MWIJAGE**





# Uteuzi wa Paul Makonda waibua hisia tofauti

- **Atumikia** uenezi CCM siku 162, Ndalichako apumzishwa

*Endelea ukurasa 5*

**MICHEZO** **GAMONDI: DK. 90 ZITAAMUA SAUZI** UK.24

**MAONI,** UK.6

# Rushwa, maslahi duni watumishi, ukatili vyateka mahubiri ya Pasaka

**Na Waandishi Wetu**

RUSHWA mahakamani na kwenye utumishi wa umma, ukatili dhidi ya wengine, maslahi duni kwa walimu na madaktari, mapenzi ya jinsia moja na tukio la mbunge kumiminiwa risasi ndio yaliyotawala mahubiri ya viongozi wa dini nchini katika Misa ya Pasaka jana.

**MALASUSA NA RISASI**

Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Alex Malasusa, katika mahubiri yake ya jana, alisema amesononeshwa kusikia Watanzania wameanza kuwindana kwa risasi kama wanyama.

Dk. Malasusa ametoa kauli hiyo siku chache baada ya Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka kudaiwa kushambuliwa kwa risasi na watu wasiojulikana.

Akihubiri katika ibada ya Sikukuu ya Pasaka katika Kanisa la KKKT Usharika wa Azania Front, jijini Dar es Salaam, Askofu Malasusu alisema:

"Tukikaribia au kusogea katika pasaka ya mwaka huu, moyo wangu umesononeka sana kusikia tena Watanzania wengine bado wanaanza kuwindana kwa kutumia risasi kama wanyama.

"Ninyi nyote mmesikia habari ya ndugu yetu Ole Sendeka, kwamba amewindwa kama anavyowindwa mnyama, na hili si tukio la kwanza.

"Na tukio hili si la kuonya, ni tukio la kukaripia, mimi nina hakika wale wenye mamlaka watalisimamia jambo hili ili Tanzamia yetu iendelee kuwa na amani kwa sababu ndio sifa ya huyu bwana aliyefufuka."

Dk. Malasusa aliwataka Watanzania kuishi kwa kujaliana na kupenda wengine, akisisitiza kuna haja ya kukemea vitendo vyote vinavyoleta au viashiria kupoteza amani nchini.

"Tuishi kwa kujali wengine. Pasaka hii itukumbushe kwamba Mungu kwa njia ya Yesu Kristo anataka tumpende yeye Mungu, lakini tupende na wengine, huwezi ukampenda Mungu na ukachukia majirani zako, ukachukia ndugu zako.

"Lakini pia tunafundishwa kuishi kwa kupenda amani, moja ya sifa ya Yesu aliyefufuka ni Mungu wa amani, tuishi kwa kupenda amani. Sifa ya mtu wa Mungu ni lazima awe balozi wa amani, na kuwa balozi wa amani ni pamoja na kukataa mafarakano yasiyo na maana au kuanzisha mafarakano yasiyo na maana," alisema

**RUSHWA**

Askofu Malasula pia alikemea vitendo vya rushwa vinavyotajwa kutamalaki katika sekta ya umma nchini, akivitaja ni vitendo vya dhuluma.



Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango akifurahia jambo wakati wa ibada ya Sikukuu ya Pasaka katika Kanisa Katoliki Parokia ya Bikira Maria Mama wa Damu Azizi ya Yesu – Kisasa Mkoani Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

"Lakini mtu yeyote anayetamani ule ulimwengu ambako Yesu anatamani sote tufike, ni lazima tukatae kutenda mambo ya kuwadhukumu wengine. Tumesikia katika nchi yetu bado rushwa inatamalaki, na wengine wanaokula na kutoa rushwa ni wakristo, hivi mnafikiri kwa kufanya hivyo si kumrudisha Yesu msalabani?

"Kwa sababu Biblia inasema 'rushwa inaleta upofu'. Kama sisi wakristo tutaona ni maisha ya kawaida, maana yake sisi pia tunashiriki. Ndugu zangu Mungu anatutamani sisi tunaomjua na kumkubali tuwe mawakala wake wa kutangaza uzuri wake," alisema.

Alisisitiza vijana kutokukata tamaa kwa sababu ya ugumu wa maisha na kuanza kufanya matendo mabaya yasiyompendeza Mungu.

"Vijana wengi siku hizi unawasikia wanasema maisha ni magumu, na juzi nilisikia eti mtoto amejinyonga kisa eti ugumu wa maisha. Ninawaomba tumtumainie Mungu, turudi kwake ndiye atatupatia majibu, ninatamani Yesu afufuke kwenye maisha ya kila mtu," alisema Dk. Malasusa.

**MASLAHI WATUMISHI**

Mkoani Kilimanjaro, akihubiri jana katika Kanisa Kuu la Usharika wa Moshi Mjini, Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini ya KKKT, Dk. Fredrick Shoo, alisema anaona hatari iliyoko mbeleni kama taifa na wenye mamlaka hawatachukua hatua za kushughulikia maslahi ya walimu na madaktari nchini.

Pia alisihi wabunge wakati wowote wanapopambana kutetea nyongeza ya mishahara na maslahi yao, wawakumbuke na wale wanaofundisha watoto wao shuleni na madaktari wanaowatibu ndugu zao na familia zao.

Alisema hana shida na mishahara ya wabunge, hata walipwe Sh. milioni 20, lakini wanapotetea maslahi yao, wawakumbuke walimu na madaktari.

"Tusipoangalia maslahi ya walimu na madaktari, ninaiona hatari, sina neno na mishahara ya wabunge. Walipwe hata (shilingi) milioni 20. Sina neno nayo.

"Walimu wanakwenda na mishahara ya 400,000. Wenye degree (shahada ya kwanza) Sh. 700,000 na madaktari hivyo hivyo. Tusiangalie maslahi yetu binafsi, tuwakumbuke na hawa.

"Wenye mamlaka, wenye nafasi nzuri serikalini, wakumbukeni hawa wanaolitumikia taifa katika kada hii. Mwalimu akikata tamaa, hali itakuwa mbaya. Mimi ninaona hapa kuna hatari kama taifa lisipochukua hatua kushughulikia jambo hili.

"Tusijilimbikizie mali, tusitamani dhuluma.Tutende kwa kadri ya faida ya taifa hili. Mnapotetea mishahara yenu na maslahi yenu, wakumbukeni wale wanaofundisha watoto wenu na madaktari," alihadharisha.

Askofu Dk. Shoo katika mahubiri yake pia alitaka wakristo na wa Tanzania kwa ujumla wake kuitumia sikukuu ya Pasaka kuitafakari na kuikataa mifumo inayosababisha maumivu, hasa ile inayokataa uzima na uhai.

Alisema kuna mifumo duniani inasababisha maumivu, hasa ile inayokataa uzima na uhai.

"Hata hapa nchini tunashuhudia vifo, ukatili na mauaji ya kinyama miongoni mwa wana familia wenyewe. Lakini pamoja na hayo yote, ufufuko wa Bwana wetu Yesu Kristo utukumbushe kutenda mwema na kuachana na mambo haya.

"Alama ya matumaini. Zawadi ya uzima wa milele, si ya kufikirika, si zawadi ya milele. Tuitumie kupata nguvu ya kusonga mbele.

"Zawadi ya matumaini haina maana tukae kimya na tukubali mateso. Tuheshimu sana uhai na kuujali sana uhai wa kila mwanadamu na viumbe vingine vyote... Maumivu, ukatili na mauaji ya kikatili vinavyotokea vitusumbue moyoni na tukatae mifumo kandamizi. Rushwa, dhuluma, ubinafsi hasa miongoni mwa wenye mamlaka vitusumbue, tuvikatae."

**UVUMILIVU KIDINI**

Askofu wa Kanisa Katoliki Zanzibar, Augustino Shao, alitaka waumini wa dini ya kikristo kuendelea kuwa na uvumilivu wa kidini kwa kuheshimu waumini wa Kiislamu wanaoendelea na ibada ya mfungo wa Ramadhani.

Alisema viongozi hao kwa nyakati tofauti wakiwa katika ibada ya Pasaka, walisema ni vyema kuendeleza utamaduni wa kuheshimiana na katika kula chakula wajihifadhi huku wakijua kuwa wenzao wanaendelea na mfungo wa Ramadhani.

Alisema maendeleo ya taifa lolote yanaletwa na watu wenyewe kwa kufuata utawala wa sheria na kwa bahati nzuri nchi huongozwa na sheria zake.

Kiongozi huyo wa kiroho alisema matamko ya viongozi si sheria, bali ni sehemu ya kujenga utulivu na amani, hivyo ni vyema vyombo vya ulinzi na usalama kusimamia haki na katiba ya nchi.

Alisema kitendo cha askari visiwani Zanzibar, kusema wako kuwasaga wanaokula mchana katika mwezi huu wa Ramadhani ni kauli potofu na za kutisha raia kwa sababu hakuna sheria katika katiba ya Tanzania na Zanzibar zinazonyima mtu kula mchana.

"Tunawaasa wanausalama wetu wasiturudishe tena kwenye utawala wa matamko, wafuate sheria zilizopo, nasi tutakuwa na amani," alisema Askofu Shao katika ibada ya sikukuu ya Pasaka katika Kanisa la Roma Shangani, mjini Zanzibar.

Alisema kwa miaka mingi dini zinaheshimiana kwa kujua kila raia ana haki ya kuabudu, na utaratibu wa kuheshimu dini ya kila mwenzake kwa kila anachoamini, kumpa fursa ya kuishi imani yake kwa amani.

"Ndio maana ndugu zangu sisi wakristo tumemaliza mfungo wetu leo, hatuna budi kusherehekea lakini kwa kuheshimu wenzetu ambao bado wako katika mfungo wao.

"Tusiwashawishi na tusiwasumbue kwa aina yoyote ile. Heshima hiyo kwetu ni neema na baraka kutoka kwa Kristu mfufuka anayetuangazia tusimtendee mwenzetu tusichopenda yeye atutendee," alisema.

Akizungumzia vitendo vya rushwa, Askofu Shao alisema ushindi wa kristu dhidi ya dhambi ni kwa sababu alitaka kujenga haki kwa wote kwamba wanadamu wote ni sawa, wanastahili heshima.

Alisema suala la rushwa nchini limerudi kwa nguvu zote kwa sababu halikemewi vya kutosha licha ya kutangazwa kuwa ni janga la taifa na kuundwa vyombo vya kudhibiti rushwa zikiwamo TAKUKURU na ZAECA, hakuna ushahidi wa wengi waliohukumiwa na kuonesha wazi kwamba rushwa ni kosa.

Askofu Shao alisema jukumu la serikali zote mbili pamoja na vyombo vyake ni kuhakikisha vipaumbele vya shughuli na ufanisi wao ni kwa wananchi wake, hivyo ziwe makini kwa swali la ajira za wageni.

"Inasikitisha ndugu zangu kuona yanayofanyika katika kivuli cha uwekezaji, nilishasema wakati fulani kwamba si rahisi kwa mtanzania akaruhusiwa kuuza ice cream pale Roma, Milano (Italia), Koln (Ujerumani), au New York (Marekani) lakini chini ya kivuli cha uwekezaji tunaona ajira za wageni za kuuza unga, sukari, kufungua mageti ya viwanda zinafanywa na wageni," alisema.

Askofu huyo alisema ni vizuri serikali zikatafari tena juu ya mikataba yake ya uwekezaji na ajira zake, hivyo uchunguzi wa kina ufanyike katika hoteli za kitalii na viwandani.

Alisema hali ilivyo haitoi matumaini kwa wasomi, hivyo serikali ziweke vigezo kwa wawekezaji wanaolipwa kwa fedha za kigeni walipwe pia vijana wa kitanzania.

Kukiwa na angalizo hilo toka kwa Askofu Shao, Askofu wa Kanisa la Anglikana, Mechaile Hafidh pia alizungumzia hoja ya kuheshimiana kiimani, akiwataka waumini kuwa na uvumilivu wa kidini na kujua kuwa wanaishi na Waislamu ambao wanaendelea na mfungo.

"Miaka yote tunaheshimiana na majirani zetu, tunajua wa-

**INAENDELEA UK. 3**

# Rushwa, maslahi duni watumishi, ukatili vyateka mahubiri ya Pasaka

**INATOKA UK. 2**

nafunga, tunaheshimiana. Kwahiyo, vyombo vya ulinzi na usalama tusibuguziane," alisema.

Pia aliwataka wananchi kuilinda na kuitunza miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na serikali kama vile ujenzi wa barabara, shule na hospitali ili kuendelea kupata mafanikio.

Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la ZICC lililoko Kariakoo, mjini Zanzibar, Dikson Kaganga pia alitaka waumini wanaposherehekea sikukuu ya Pasaka kuheshimu wengine bila ya kuvunja sheria.

Alisema bila kuwapo uhuru wa kuabudu, amani na usalama utakosekana na Tanzania ina uhuru wa kuabudu, hivyo ni vyema kuvumiliana, zikiwa zimebaki siku 10 kumaliza mfungo wa Ramadhani, kula hadharini kutarejea Zanzibar.

"Serikali haijazuia mtu kula, hata mimi asubuhi nimekula kwangu nikiwa ndani, na ninachofahamu kwamba serikali imetoa tahadhari kwamba tusile mchana hadharani kwa sababu wengine wapo katika mfungo na pengine kwa imani yao kula mchana hadharani kunaathiri funga zao, tuvumiliane ili tuishi kwa amani, upendo na mshikamano," alisema.

Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Efadha Zanzibar, Herry Nelson alisema Tanzania ni nchi ya amani na wasisi wa taifa hilo wamewajenga wananchi katika umoja bila ya ubaguzi wa kidini na kila mwananchi asimamie misingi ya dini yake.

**RUSHWA KORTINI**

Askofu wa Kanisa la Anglikana Tanzania Dayosisi ya Kati (DCT), Dk. Dickson Chilongani alimwomba Rais Samia Suluhu Hassan kutupia macho suala la rushwa, akisisitiza bado linatajwa kwa kiwango kikubwa hasa mahakamani.

Dk. Chilongani alisema "Kama Mwalimu Nyerere alivyosema rushwa ni adui wa haki, tusingependa iendelee kuota mizizi katika maeneo nyeti ya nchi yetu kama vile mahakamani," alisema.

Alipongeza Rais Samia kwa kuimarisha demokrasia na utawala bora nchini na tangu aingie madarakani amekumbatia watu wa dini na vyama vya siasa na nchi haijateteleka na amani imeendelea kushamiri tofauti na baadhi ya nchi.

Askofu Chilongani alisema "Tunapoelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu, ni vyema kuwe na usawa, tuwaamini wanawake.

"Yesu aliwafanya wanawake kuwa mashahidi kwa kufufuka kwake, kupitia kifo chake na kufufuka kwake Yesu anafanya mageuzi ya kuvunja ukuta uliomtenga mwanamume na mwanamke na kumfanya mwanamume ajione bora zaidi kuliko mwanamke badala yake Yesu anataka mwanamume na mwanamke wote wajione wako sawa," alisema.

Akitoa salamu katika ibada hiyo, Waziri Mkuu mstaafu, John Malecela, aliasa waumini kutumia sikukuu hiyo kutambua wako huru na wamesamehewa.

"Kama kuna mtu ambaye nilimkosea anisamehe na mimi nitamsamehe aliyenikosea," alisema.

Mkuu wa Majeshi, Jenerali Jacob Mkunda, alisema serikali iko imara na kuhakikishia Watanzania kuwa nchi iko salama.

"Mataifa mengi yameshindwa kusherehekea siku hii kwa kukosa amani, rai yangu mimi kwa Watanzania tuidumishe amani iliyopo.

"Kuna watu nchi nyingine wanashindwa kusherehekea kwa sababu hawana amani, tushikilie amani tuliyonayo. Mwaka huu kuna Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na mwakani Uchaguzi Mkuu, hivi vyote vinapaswa kufanyika na kulinda amani iliyopo," alisema.

Jenerali Mkunda alisema maendeleo ya nchi yoyote yanatokana na amani iliyopo, hivyo Watanzania wailinde na kuidumisha.

**MAKAMU WA RAIS**

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na mkewe, Mbonimpaye Mpango waliungana na waumini mbalimbali kushiriki ibada ya sikukuu ya Pasaka katika Kanisa Katoliki Parokia ya Bikira Maria Mama wa Damu Azizi ya Yesu - Kisasa Mkoani Dodoma.

Akitoa salamu za sikukuu ya Pasaka mara baada ya kushiriki ibada hiyo, Makamu wa Rais alitoa wito kwa Watanzania kutumia sikukuu ya Pasaka kutambua hakuna ushindi bila kujitoa kwa ajili ya wengine; familia, wahitaji na taifa.

Alisema ni lazima kujitoa kwa kutimiza wajibu vizuri kwa kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya maendeleo ya nchi ya sasa na vizazi vijavyo.

Makamu wa Rais alisema ni muhimu kutumia sikukuu ya Pasaka kujifunza kushinda ubinafsi na kuhakikisha haki na huduma zinatolewa bila kuomba rushwa.

Makamu wa Rais pia aliagiza viongozi na watumishi wa serikali kuwa kielelezo cha kujitoa kwa ajili ya kutumikia watu wengine.

Ibada hiyo iliongozwa na Padre Vedastus Ngowi kwa kushirikiana na Paroko wa Parokia hiyo, Sostenes Ndendya.

**UKATILI**

Askofu wa KKKT Dayosisi ya Dodoma Christian Ndosa, aliwataka Watanzania kujiepusha na vitendo vya kikatili na badala yake waendele kumwomba Mungu kudumisha amani iliyopo nchini.

***SOMA HABARI ZAIDI UK. 4**

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**SADOTH MUTATINA BANOBENJU** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YAKE YA GARI LENYE NAMBA ZA USAJILI **T 480 DCQ**. AMETOA TAARIFA POLISI NA KUPEWA NAMBA **PHQ/KAG/BUK/3245/2024.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI AU APIGE SIMU NAMBA **0764070980.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**
**WAKALA WA TAIFA WA HIFADHI YA CHAKULA**
Kizota Viwandani Area | S.L.P 1050 Dodoma | Simu: +255(0)26 2963953 | Fax:+255(0)26 2963950
Barua pepe: info@nfra.go.tz | Tovuti: www.nfra.go.tz

NFRA

## TANGAZO KWA UMMA

## MIKATABA YA UNUNUZI WA MAHINDI MEUPE (NON-GMO) NA MPUNGA

Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ni Taasisi ya Serikali chini ya Wizara ya Kilimo. NFRA imeanzishwa chini ya Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya mwaka 1997 kwa madhumuni ya kuhakikisha usalama wa chakula Nchini. Katika kutekeleza moja ya majukumu yake, NFRA hununua nafaka kwa ajili ya Akiba ya Taifa ya chakula.

NFRA inatarajia kununua Mahindi Meupe na Mpunga katika msimu wa ununuzi wa mwaka 2024/2025, kuanzia tarehe 1 Julai, 2024. Ununuzi huo utafanyika kwenye maghala yaliyopo kanda za Arusha (ghala la Arusha na Babati), Dodoma (ghala la Dodoma na Manyoni), Kipawa (Dar es Salaam), Makambako, Songwe, Shinyanga, Songea na Sumbawanga (Sumbawanga na Mpanda) na vituo vingine ambavyo vitafunguliwa na Wakala.

Aidha, ili kuongeza wigo wa kufikia ununuzi wa tani 700,000 pamoja na kuwa na utaratibu wenye tija katika shughuli za ununuzi msimu wa 2024/2025, NFRA itaingia Mikataba ya Ununuzi wa nafaka (Framework Agreement) na Wakulima pamoja na Wafanyabiashara wenye sifa zilizoainishwa hapa chini.

1. **MASHARTI KWA MKULIMA:**

   i) Mkulima awe na shamba kuanzia ekari 100 ndani ya eneo moja katika Halmashauri/Wilaya na kuwepo na uthibitisho huo kutoka Serikali ya Kijiji/Halmashauri ya Wilaya ya shamba lilipo.

   ii) Mkulima awe na uwezo wa kuzalisha kuanzia tani 200 za Mahindi Meupe au Mpunga.

2. **MASHARTI KWA MFANYABIASHARA:**

Mfanyabiashara lazima atimize masharti yafuatayo;

a. Awe na uwezo wa kuiuzia NFRA kuanzia tani 2,000 hadi 5,000 za Mahindi Meupe au Mpunga.
b. Hati hai ya kutodaiwa kodi (valid tax clearance)

3. **MASHARTI YA UJUMLA:**

   i) Mwombaji anapaswa kuwasilisha uthibitisho wa; -
   a. Uraia au kampuni iliyosajiliwa Tanzania;
   b. Namba ya Mlipa Kodi (TIN) na kuwa tayari kulipa kodi za Serikali;
   c. Leseni ya biashara ya mazao;
   d. Barua ya utambulisho kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri wa eneo ambalo Muombaji anafanya shughuli zake za kilimo au biashara;
   e. Utayari wa kuridhia kuuza nafaka yake kwa bei itakayopangwa na NFRA;
   f. Utayari wa kuridhia kuwasilisha Mahindi au Mpunga katika ghala/kituo atakachoelekezwa na kwa muda atakaopangiwa kwa mujibu wa Mkataba atakaoingia na NFRA;
   g. Mahali salama pakuhifadhia Mpunga au Mahindi Meupe kabla ya kununuliwa na NFRA;
   h. Kuzingatia vigezo vya ubora wa Mpunga na Mahindi Meupe daraja la kwanza vilivyowekwa na NFRA kwa mujibu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

   ii) Mwombaji anaelekezwa kuwasilisha barua ya maombi ya kuiuzia NFRA Mpunga au Mahindi Meupe kabla au ifikapo tarehe 20 Aprili, 2024. Barua husika iwasilishwe kwa Mameneja wa Kanda kwa njia ya barua pepe au anuani za ofisi za Kanda zilizokaribu na Mwombaji au anapokusudia kuwasilisha nafaka zake.

   iii) Barua ya maombi iainishe yafuatayo; jina na anuani ya mwombaji, namba ya simu, baruapepe, kiasi cha Mpunga au Mahindi Meupe anayokusudia kuuzia NFRA na kituo anachopendekeza kuwasilisha Mpunga au Mahindi Meupe.

   iv) Waombaji watakaofuzu vigezo na masharti wataingia mikataba na NFRA ya kuuza Mpunga au Mahindi Meupe kwa kuzingatia uhitaji wa nafaka kutoka kwa NFRA (framework contract), kuanzia tarehe 1 Mei 2024.

Tanbihi: Mkulima/Mfanyabiashara asiye na vigezo tajwa hapo ataendelea kuuza nafaka zake kwa kuwasilisha katika maghala makuu ya NFRA yaliyopo katika Ofisi za Kanda au vituo vya ununuzi vitakavyofunguliwa na NFRA, pasipo kuwa na mikataba hii ya ununuzi kutoka NFRA.

Kwa taarifa zaidi Mwombaji anaweza kuwasiliana na NFRA kupitia **simu namba +255 (0) 26 2963953** au Baruapepe: **info@nfra.go.tz**

**Imetolewa na:**
**Afisa Mtendaji Mkuu,**
**Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula**
**Tarehe 25 Machi, 2024.**

# Maaskofu wakemea ndoa za jinsia moja

**Na Waandishi Wetu**



Mkuu wa Jimbo la Tumaini na Usharika wa kanisa la kiinjili la kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mufindi, Mchungaji Baraka Mbangula akipokea zawadi ya mshumaa kutoka kwa marafiki zake toka nchini Ujerumani waliofika kanisani hapo kushiriki Ibada ya Pasaka jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

KATIKA kuadhimisha misa takatifu ya sikukuu ya Pasaka, maaskofu katika maeneo mbalimbali nchini wamekemea vikali vitendo vya kikatili vinavyosababishwa na imani za kishirikina dhidi ya watoto, wanawake na wazee.

Pia wamesisitiza suala la maadili katika familia ikiwa ni pamoja na kukemea na kudhibiti ndoa za jinsia moja zinazozidi kushamiri katika jamii.

Askofu wa Jimbo Katoliki Shinyanga, Mhashamu Liberatus Sangu, akihubiri katika Mkesha wa Pasaka uliofanyika katika Kanisa Katoliki Parokia ya Ngokolo, Manispaa ya Shinyanga, alisema pasaka ni kukombolewa kutoka kwenye utumwa wa dhambi.

Alisema Kristo alifia dhambi za wanadamu na kuifungua milango ya mbinguni ambayo ilikuwa imefungwa kutokana na dhambi, hivyo kuwataka watu kuacha kutenda maovu, ikiwa ni pamoja na utoaji mimba.

"Tuuvue utu wa kale tuvae utu mpya, acheni uasherati, uzinzi, ushirikina, ugomvi, mauaji na kutoa mimba kwani yote ni machukizo kwa Mungu. Wakumbukeni pia yatima na wajane, mnapowatendea mema, mnamtendea Yesu Kristo," alisema Askofu Sangu.

Alitumia misa hiyo kuliombea taifa pamoja na viongozi wote ili waendelee kudumisha na kusimamia amani hususani kuelekea uchaguzi wa ngazi mbalimbali na kuwaita waamini wenye sifa za kugombea nafasi hizo kuzitumia vizuri.

Pia aliwataka Watanzania kutokudanganywa kwa rushwa katika kipindi cha uchaguzi na kupoteza haki zao, bali wapokee fedha na vitu hivyo na kuwaangusha katika sanduku la kula.

"Wakikuletea wewe pokea tu, weka mfukoni, kula lakini kwenye kura wapige chini. Hapa niwaombe wagombea wanaotumia rushwa kutafuta kura, huo si uzalendo, ni ubinafsi. Niwakumbushe wale wenye uwezo wa kugombea nafasi tumieni wakati huo kuonesha uwezo wenu ili kuzikomboa jamii zenu," alisema.

Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Tabora, Mwadhama Kardinali Protase Rugambwa, akiongoza misa hiyo jana, alihimiza waumini tutokukaa katika giza la maisha pale wanapokumbana na matatizo mbalimbali katika maisha yao na kuhakikisha wanayakabilia kupitia maombi kwa Mungu.

Pia aliwataka kutokukata tamaa wakati wote wanapokumbana na majaribu, bali kupitia maombi kwa Mungu ili wayashinde na kupata ushindi wa milele.

"Tujifunze kutoka kwa Kristo mfufuka juu ya neema ya kupenda na kusamehe hata kutokukata tamaa mpaka pale alipotekeleza adhima yake ya kukomboa ulimwengu kutoka kwenye dhambi," alisema Kardinali Rugambwa.

### NDOA JINSIA MOJA

Askofu wa Jimbo Katholiki Bukoba, mkoani Kagera, Jovitus Mwijage alihimiza kinamama kuwa waombezi wa familia zao kutokana na wao kupewa kipaumbele cha kushudia ufufuko wa Yesu Kristo kaburini.

Askofu Mwijage alisema kwa neema hiyo na maagizo yaliyotolewa na Yesu Kristo wakati wa mateso yake, wanawake wanapaswa kuwa wasimamizi wazuri wa maadili na mienendo mizima katika familia, ndoa na watoto na kuwadhibiti kwenda kinyume cha maadili.

"Matukio mengi yanayokwenda kinyume cha maadili na imani ikiwamo mavazi yasiyofaa, kuvaa mavazi ya jinsia tofauti yanayoashiria vitendo vya mapenzi ya jinsia moja. Ukiona binti yako au kijana amevaa nguo ambayo si yake, kaa naye umwonye, umrudishe katika mstari.

"Utaona sasa wavulana wametoboa masikio, wamevaa suruali iko chini, hiyo kwa nchi nyingine ukiona mtu amevaa hivyo, huyo anakuwa ni shoga, mkanye mtoto mapema," alisisitiza Askofu Mwijage.

Askofu Mstaafu Jimbo Kuu Katoliki la Bukoba Mhashamu Methodius Kilaini, pia alisisitiza umuhimu wa maadili mema kwa watoto, akihimiza kuwalea kwa kuzingatia mafundisho ya dini na kuacha kiburi ambacho kimekuwa kinasabisha kukosa heshima kwa wazazi na kufuata mambo yasiyofaa katika jamii.

"Lazima tukumbuke kuwa katika maisha yetu ya kila siku kitu kizuri kinalipa na vilevile kitu kibaya kinaharibu, hivyo jiandae kuharibu pale unapotenda mabaya na kulipwa pale unapotenda mema," alisema Askofu Kilaini. Askofu wa Jimbo Katoliki la Mbulu, Antony Lagwen pia alikemea vitendo viovu vya ndoa za jinsia moja, ulawiti na ubakaji katika jamii, akisisitiza havikubaliki kwa mtu yeyote, vipingwe kwa nguvu zote.

"Ndugu zangu tusikubali kufumbia macho ushoga, ulawiti na ubakaji, tuvipinge kwa nguvu, mtu yeyote anayetaka twende huko tusimsikilize, amejaa uovu, bali tumkimbilie Yesu aliyefufuka leo," alisema.

Ni vitendo vilivyokemewa pia na Naibu Katibu Mkuu Misioni ya Uinjilisti ya Dayosisi ya Kaskazini Kati ya KKKT, Julius Laizer, aliyesema Watanzania wanapaswa kupambana na kupiga vita matendo machafu ya ushoga, usagaji, ndoa za jinsi moja, ulawiti na ukatili wa kijinsia.

### MINDE NA USASA

Askofu wa Jimbo Katoliki la Moshi, Mhashamu Ludovick Minde, alisema kiini cha vijana wengi nchini kupoteza uwezo wa kufikiri, kusema, kushirikisha mambo, kutenda na mwenendo mzima wa maisha yao ni 'usasa' unaochagizwa na ukuaji wa sayansi na teknolojia.

"Kwa sasa wimbo uliopo duniani ni kuporomoko maadili kwa vijana na watoto. Je, sisi wazazi na walezi tumejitafakari nini chanzo cha haya?

"Jibu ni kila mmoja kushindwa kujifungamana na Yesu na badala yake kujikita katika mambo ya kidunia. Haifai, haipendezi, tubadilike!" Askofu Minde alionya.

"Ninapotoa salama za pasaka, ninaomba niwaalike nyote kuwa wapya na kuyatafakari maisha yetu, tuache kuendelea na utandawazi na badala yake turudi nyumbani kwa Yesu Kristo, ili kufurahia matunda ya upendo, msamaha, ukweli na kuwa tayari kubebeana upungufu kwa ajili ya mwenzio.

"Haya mambo ya kulipiza kisasi, kuwaua watoto, ndugu na wazazi ili tupate fedha si yetu. Tubadilike tunakoenda siko," alihadharisha.

### UCHAGUZI MITAA

Mkoani Iringa, Askofu wa KKKT Dayosisi ya Mufindi, Dk. Antony Kipangula alitaka Watanzania kuendelea kuomba ili Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika mwaka huu ufanyike salama, pia kuombea maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwakani ili kupata viongozi wenye hofu ya Mungu.

Katika salamu zake za Pasaka huko Mafinga, Askofu Kipangula alisema Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ni muhimu kwa nchi, hivyo lazima maandalizi yake yaende sambamba na maombi ili kupata viongozi wenye hofu ya Mungu.

Alisema uchaguzi huo utaunda serikali kwa ngazi za vijiji na mitaa, hivyo iwapo watapatikana viongozi wasio na sifa itakuwa mzigo Kwa taifa.

"Lazima viongozi wenye sifa wapatikane ili kuja kupata madiwani, wabunge na Rais mwenye hofu ya Mungu kwenye Uchaguzi Mkuu mwakani," alisema na kutoa rai kwa wale wenye sifa kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali badala ya kuwa watazamaji na kuwaachia wale wasio na sifa.

Askofu Dk. Kipangula pia alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan Kwa kuendelea kuchukizwa na vitendo vya ufisadi nchini.

Alisema ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na ile ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ambazo Rais Samia alikabidhiwa Alhamisi iliyopita, zimeonesha kiongozi huyo anachukizwa na matumizi mabaya ya fedha za umma.

"Maagizo ya Rais Dk. Samia kwa wale wanaohusika na upotevu wa fedha za umma ni vyema yakafanyiwa kazi ikiwa ni pamoja na wahusika kuchukuliwa hatua kali," alisema.

Kuhusu dayosisi hiyo mpya ya Mufindi, alisema kwa sasa kanisa linaendelea kupanga vyema safu ya viongozi watakaoongoza kwa kipindi cha miaka mitano.

***Imeandaliwa na Vitus Audax (MWANZA), Marco Maduhu (SHINYANGA), Restuta Damian (KAGERA), Oscar Assenga (TANGA), Allan Isack (ARUSHA), Mary Mosha (MOSHI) Steven William (MUHEZA), Mariam Bole (SAUT), Jaliwason Jasson (MANYARA), Elizabeth Zaya (DAR), Godfrey Mushi (MOSHI) na Rahma Suleiman (ZANZIBAR).**

HABARI KITAIFA

# Panga, pangua ya Rais Samia

## -Siku 162 Ukatibu Itikadi na Uenezi wa Makonda waacha gumzo

**Na Mwandishi Wetu**

NI siku 162 za Paul Makonda kushika nafasi ya Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), ambazo alizitumia kufanya ziara kwenye mikoa mbalimbali nchini, kutoa matamko mazito na kuwawajibisha viongozi mbalimbali wakiwamo mawaziri.

Siku hizo zinatimia baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, (pichani) usiku wa kuamkia jana (saa 6.06 wakati taarifa inatolewa) kumteua kuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, akichukua nafasi ya John Mongella ambaye atapangiwa kazi nyingine.

Alipoteuliwa kushika nafasi ya Katibu wa Itikadi na Uenezi, alianza ziara ya siku saba katika mikoa ya Kanda ya Ziwa Novemba 9 hadi 14, mwaka 2023 ambako alionyesha kutoridhishwa na utendaji wa watumishi wa umma huku akiwapigia simu mawaziri akitaka majibu ya changamoto za wananchi.

Aidha, alifanya ziara Mkoa wa Dar es Salaam katika wilaya mbalimbali na baadaye alielekea Kanda ya Kaskazini ambako aliendelea na kusikiliza kero za wananchi na kuwapigia viongozi wa juu kupata ufumbuzi wa kero za wananchi.

Katika mikoa yote aliyotembelea, Makonda alisikiliza kero za wananchi na wengi wao kukimbilia ziara zake kwenye kituo kinachofuata ili kueleza changamoto wanazopitia na kutotatuliwa na mamlaka zilizopo.

Kila mkoa aliokwenda kiongozi huyo alitumia usafiri wa aina tofauti kama pikipiki, guta, bajaji, buldoza, farasi, baiskeli na trekta ikiwa ni namna ya kuteka wafuatiliaji wa siasa za CCM.

Baada ya taarifa ya Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu, kutangaza uamuzi wa Rais Samia kufanya mabadiliko madogo kwenye Baraza la Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakuu wa mikoa na wilaya, mjadala mkali uliibuka mtandaoni kuhusu Makonda kama amepanda au ameshushwa cheo.

Mjadala mwingine ni wa waziri wa muda mrefu tangu serikali ya awamu ya tano, Prof. Joyce Ndalichako, ambaye alikuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) na nafasi yake kuchukuliwa na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI),Deogratius Ndejembi.

Prof. Ndalichako ni Mbunge wa Jimbo la Kasulu huku aliyechukua nafasi yake ni Mbunge wa Chamwino.

**MAONI YA WADAU**

Katika ukurasa wake wa X (zamani Twitter) Mbunge wa zamani wa Arusha (CHADEMA), Godbless Lema, aliandika ujumbe akiwatakia watu wa Arusha heri ya Pasaka.



Sehemu ya ujumbe huo unasomeka: "Sisi ni washindi wakuu katika kila hatua na kama kuna kusudi baya juu yetu, basi kuweni na amani sana kwamba hawatafanikiwa hata kwa nukta moja.

"Kila kikao kitakachokaa kwa mipango mibaya kitasambaratika na wapangaji mtawatafuta na wala msiwaone.

"Naona mna wasiwasi kwa sababu ya historia. Kuweni na amani sana na mjue Mungu yuko kazini na sisi tuko na imani ya kuwashinda waovu wote bila kuangalia nafasi zao."Mwenyekiti wa Mpito wa NCCR-Mageuzi, Joseph Selasini, kwenye andiko lake katika moja ya kundi sogozi la Whatsapp ameandika, "Tambueni huu ni mwaka wa uchaguzi. Teuzi zote zinaangazia uchaguzi."

Mwenyekiti wa Wafanyabiashara Wilaya ya Arusha, Dominic Mollel, alisema uteuzi wa Makonda kuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, ana imani unalenga kurejesha imani yao hasa kutokana na mioyo ya baadhi yao kumeguka.

Yohana Msita aliandika katika ukurasa wa X wa Ikulu: "Watanzania wengi bado hawamuelewi Mama yetu Rais Dk. Samia, sifa mojawapo ya kiongozi, usiinue mabega, usitishie maisha wengine, uwe shirikishi, usitafute sifa za kijinga, tenda haki na uwe mwaminifu na mwadilifu Tanzania sio shamba la bibi hata kidogo."

Mwingine aliyejitambulisha kwa jina la Mageuzi. A. Mwang'onda Jr aliandika: "Niseme ukweli ila sitasema kwa upande gani ila Mh. Dk. Samia una jicho mama hongera Mwenyezi Mungu aendelee kukujalia afya njema, umri mrefu mama angu, hongera hongera huu mkeka wa leo mama una jicho maana nilianza kuona jambo haliendi sawa."

Amosi Lugimba aliandika "Hongera sana kwa wanaoendelea kuaminiwa na serikali. Wakafanyekazi na kuweka maslahi ya taifa kwanza, huku wakiilinda imani ya Mh. Rais Dk. Samia Suluhu Hassan."

George Karwani aliandika: "Mh. Rais, mama yetu! Mimi kama mwana CCM na mkazi wa Arusha tunakushuruku sana kutupatia jembe Mh. Makonda, kijana mchapakazi, mwenye moyo mpana wa uzalendo. Mh. Makonda karibu sana Arusha kazi iendelee."

Evaristo Brighson aliandika: "Mama kuna wakuu wa mikoa wapo mikoa hiyo hiyo muda mrefu huku wengine kila baada ya mwaka unawahamisha, ikikupendeza wale waliokaa mkoa mmoja muda mrefu wapeleke mikoa mingine wapeleke uzoefu wao au kupata changamoto mpya ili kuondoa mazoea."

Wengine walioteuliwa na Rais Samia ni Kanali Evans Mtambi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mara ambaye kabla ya uteuzi alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Mkinga.

Aidha, Rais Samia amemhamisha Said Mtanda kutoka Mkoa wa Mara kwenda kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza akichukua nafasi ya Amos Makalla, ambaye atapangiwa kazi nyingine.

Pia amemteua Zainab Katimba kuwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa ana Serikali za Mitaa (TAMISEMI) akichukua nafasi ya Deogratius Ndejembi ambaye ameteuliwa kuwa Waziri.

Daniel Sillo ambaye ni Mbunge wa Babati Vijijini ameteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi akichukua nafasi ya Jumanne Sagini ambaye amehamishwa kwenda kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria.

Mhandisi Maryprisca Mahundi ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum amehamishwa kutoka Wizara ya Maji kwenda kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari huku akimhamisha Kundo Mathew ambaye ni Mbunge wa Bariadi kutoka wizara hiyo kwenda kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maji.

Fakii Lulandala ameteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, kabla ya uteuzi alikuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM). Gilbert Kalima amekuwa Mkuu wa Wilaya ya Mkinga ambaye kabla ya uteuzi huo alikuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi CCM.

Mhandisi Cyprian Luhemeja amehamishwa kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Wenye Ulemavu) kwenda kuwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).

Pia, amemhamisha Mary Maganga kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwenda kuwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), huku akimteua Dk. Edwin Mhede kuwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambaye aliwahi kuwa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), akichukua nafasi ya Agnes Meena anayekuwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maji.

Dk. Suleiman Serera ameteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kabla ya uteuzi alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, anachukua nafasi ya Nicholaus Mkapa ambaye amehamishwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia wa Habari.

Selestine Kakele ameteuliwa kuwa balozi, kabla ya uteuzi huo alikuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, huku akimteua Balozi Dk. Asha Rose Migiro kuwa Mjumbe wa Tume ya Mipango.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa uapisho wa Waziri, Wakuu wa Mikoa, Naibu Mawaziri na Naibu Makatibu Wakuu utafanyika Aprili 4, mwaka huu majira ya saa 5:00 asubuhi, Ikulu ya Dar es Salaam.

# Zitto: Lazima Tanzania ibadilishe mifumo ya uchaguzi

**Na Maulid Mmbaga**

ALIYEKUWA kiongozi wa chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema ni lazima Tanzania ibadilishe mifumo yake ya uchaguzi, kwa kuwa Rais ameshatia saini Sheria ya Tume ya Uchaguzi na kwamba ni busara Tume ya sasa ijiuzuru ili kutoa nafasi ya kupata mpya.

Alisema kwa kuwa sheria mpya imetoa utaratibu bora wa kupata makamishna wa Tume kuanzia mwenyekiti, walioko sasa wanapaswa kuachia ngazi ili ianze kufanya kazi yake na kutoa mfano wa Senegal katika nchi za Afrika kuendesha uchaguzi vizuri.

Mwanzilishi huyo wa ACT-Wazalendo aliyasema hayo jana wakati akizungumza na chombo kimoja cha habari baada ya kurejea kutoa nchini Senegal ilioyokuwa ikiendesha uchaguzi wa urais siku chache zilizopita.

Zitto ni miongoni mwa wanachama walioko kwenye Mtandao wa Viongozi wa Kisiasa wa Vyama Pinzani Afrika, ambao ulikuwa nchini Senegal kushughudia uchaguzi wa urais.

Akizungumzia matamanio yake alisema, anataka kuwa rais, wakati gani, inategemea na mazingira ya kisiasa na majaliwa ya Mungu, kwa kuwa anaweza kutaka na asipate na wala asiwe na uhuru, licha ya kueleza kwamba uchaguzi wa 2025 atakwenda kuomba ridhaa ya kurejea bungeni.

"Sababu ya kutaka kuwa rais naamini kwamba nina maarifa ya kutosha ya kuweza kuisogeza nchi yetu kuwa mbele zaidi na ninaamini kwamba nchi yetu inastahili mabadiliko, hatuwezi kuendelea kuwa na chama kile kile toka nchi ipate uhuru, tukategemea tutapata mabadiliko," alisema Zitto.

Alisema Tanzania inahitaji mabadiliko ya kisiasa, na lazima mbadala uwe ni chama ambacho kinaweza kikatatua changamoto za kimaendeleo, pamoja na umasikini.

Zitto alisema endapo atafanikiwa kuwa rais ajenda yake kubwa itakuwa ni kupambana na umasikini, akieleza kwamba anachukizwa kuona miaka yote toka wamepata uhuru, karibu theluthi ya Watanzania wanaishi chini ya mstari wa umasikini.

Akizungumzia uchaguzi wa nchini Senegal, alisema toka mwaka 2000 mpaka sasa kumekuwa na mabadiliko, na kwamba vyama vitatu tofauti vinaongoza katika taifa hilo, akieleza kuwa hiyo inaonyesha ukomavu wa demokrasia.

"Kule Senegal ukimaliza tu kupiga kura, pale pale baada ya kuweka kila kitu sawa kura zinahesabiwa wazi wazi, masharti ya kuambiwa kaa mita 200 hakuna, ukimaliza kupiga kura ukitaka kubaki unabaki na karatasi inatolewa inaonyeshwa, kuna ujumbe mkubwa sana katika huu uchaguzi wa Senegal katika maeneo yote ya bara la Afrika," alisema Zitto.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga nafasi bado ipo nusu fainali mechi CAF

**AFRIKA** na dunia kwa ujumla imeshuhudia wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba na Yanga wakimaliza dakika 90 za kwanza nyumbani, moja ikipoteza kwa bao 1-0 Ijumaa iliyopita, na nyingine juzi, Jumamosi ikitoa suluhu.

Simba, ikiwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, ilikubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Mabingwa Watetezi, Al Ahly ya Misri Ijumaa na Jumamosi, Mabingwa wa Tanzania Bara, Yanga wakitoka suluhu dhidi ya Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini.

Kila mtu aliyeshuhudia mechi hizo aliona uwezo wa timu za Tanzania kupambana na miamba inayoongoza kwa ubora Afrika na kutisha barani humu.

Simba ilitawala karibuni mchezo mzima na kilichokosekana ni utulivu kwa wachezaji wake kuuweka mpira wavuni. Pia bao lililofungwa lilikuwa makosa ya mchezaji mmoja na wala si ya kimfumo.

Kwa siku za hivi karibuni, Simba imekuwa ikiruhusu mabao kutokana na makosa ya mara kwa mara ya kujirudia ya mabeki wake hasa wa kati ambao wamekuwa na tabia ya kutaka kucheza zaidi na jukwaa kuliko kucheza kama mabeki asilia wanavyotakiwa wawe.

Mabeki kiasili ni mchezaji ambaye kazi yake ni kuzuia hatari zinazoelekezwa langoni mwake, lakini pia kosa moja kubwa kwake ni kukaa na mpira muda mrefu bila sababu yoyote eneo la langoni mwao, au kutaka kupiga chenga isiyokuwa na sababu yoyote.

Ni wazi Fondoh Che Malone na mwenzake, Henock Inonga wamekuwa wakifanya makosa mengi kwenye kikosi cha Simba na kusababisha madhara na hata mabao yanayoweza kuepukika kwa kushindwa kujua ni muda gani wa kukaa na mpira na muda gani hakuna haja ya mpira kuwa eneo la hatari.

Mfano kukikuwa na wachezaji wengi wa upinzani langoni na tukio ni la kushambuliwa, mpira hautakiwi uwe eneo hilo, unapookolewa unatakiwa haraka uondoke kwenye eneo la hatari.

Kitendo cha kutuliza na kuupaka rangi kutaka kupiga chenga au kutoa pasi fupi eneo hilo hilo, unakaribisha hatari langoni.

Nadhani mabeki wa Yanga wanafundishwa vizuri sana kuhusu hilo, ndiyo maana huwa wakati wa kukaa na mpira wakakaa nao na wakati wa kuokoa uende mbali wanafanya hivyo.

Timu zote mbili zitakwenda kucheza mechi ugenini, Aprili 5, Simba ikiwa Cairo na Yanga Afrika Kusini. Kwa jinsi zilivyocheza timu hizo za Tanzania zinaweza kabisa kushinda mechi zao ugenini na kutinga hatua ya nusu fainali. Simba kwa jinsi ilivyocheza na kwa hivi karibuni imekuwa ikicheza mara kwa mara na Al Ahly, inaweza kabisa kucheza ugenini chini ya shinikizo la mashabiki wa timu pinzani Cairo na kushinda.

Ina wachezaji wazoefu, wenye uwezo wa kucheza popote pale na wakapata matokeo kama watatulia na kutumia nafasi nyingi wanazozitengeneza, lakini pia kama mabeki wake wataacha kutengeneza makosa wenyewe yanayosababisha waruhusu mabao tunaamini inaweza kupindua meza.

Kama ilicheza mbele ya mashabiki wa Wydad Casablaca nchini Morocco msimu uliopita na kuwafanya wageuze uwanja sehemu ya kuomba Mungu, basi wanaweza pia kuwafanyia Wamisri hao wakiwa Uwanja wa Cairo. Yanga ambayo yenyewe inahitaji ushindi au sare ya mabao ili kufuzu, ina nafasi nzuri zaidi.

Uzuri wa timu hiyo kunakuwa na uhakika wa mabeki wake kutoruhusu bao kwa dakika 90 kwa sababu hawana mbwembwe, kwa hiyo kinachotakiwa ni safu yao ya ushambuliaji kusaka bao angalau moja ugenini ili kuwaweka Mamelodi kwenye mazingira magumu.


Cha kushukuru zaidi katika mechi hizi hakukuwa na idadi ya mabao mengi, hivyo timu zote zina nafasi ya kuweza kusonga mbele.

Simba ina uwezo wa kupindua meza, kama nilivyosema wakiweza kutumia nafasi zao vema wanazotengeneza, hivyo zikijipanga vizuri tu kuanzia kwa viongozi, makocha na wachezaji, zinaweza kabisa kusonga mbele kitu ambacho Watanzania kwa ujumla wanataka kuona kikitokea katika historia ya soka la nchi hii kwa zote kutinga nusu fainali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Yanga achaneni na tabia ya kuingiza mashabiki bure

**IMEKUWA** ni utaratibu wa Klabu ya Yanga mara kwa mara hasa inapokuja mechi ya kimataifa kuingiza mashabiki bure.

Ni utaratibu ambao una faida, lakini mara nyingi umekuwa na hasara kwa watu wengine na hasa mashabiki hao hao wanaokuja kuingia bure.

Mara nyingi mageti huvunjwa na kuisababishia hasara serikali, na hata kwenye mechi ya Jumamosi kati ya Yanga dhidi ya Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini kumeshuhudiwa uvunjaji wa mageti na uharibifu mwingine ambao mpaka sasa bado haujaripotiwa.

Watu walikuwa wanaingia kwa kusukumana na kukanyagana na kusababisha madhara ambapo taarifa za awali zinasema baadhi yao walikimbizwa hospitali.

Binafsi, sipingi watu kuingia bure, lakini ili mashabiki waingie bure, usimamizi wake unatakiwa uwe mkubwa zaidi, usalama nao unatakiwa uwe wa hali ya juu kiasi kwamba gharama za uendeshaji zinakuwa kubwa zaidi tofauti na wakiingia kwa kulipa kiingilio.

Nafahamu, mimi mwenyewe naishi uswahilini, zinapotangazwa mechi za bure, wanaokwenda uwanjani si watazamaji wema tu, bali hata wale ambao kazi yao ni wizi, kukaba, kupora nao wanakwenda ili kutumia fursa hiyo kufanya kazi zao chafu. Watachanganyikana na watu wema na kufanya kazi yao iliyowapeleka huko.

Mechi inapokuwa ya bure hata ustaarabu pia hutoweka kwa sababu baadhi ya watu wanaokwenda uwanjani, si tu kwamba si mashabiki wa soka, lakini wengine hawajawahi hata kuingia uwanjani, hawajui hata pa kuingilia wapi, badala yake wanataka kuingia popote pale wanapoona kuna mlango.

Kuna wengine wanaingia na kutaka kwenda kukaa popote pale, hata sehemu ambayo hawatakiwi, badala yake wanawafanya mashabiki wengine wasiwe huru, baadhi kukosa kabisa pa kukaa.

Achilia mbali kuvunja mageti, wengine wanakwenda vyooni kuchomoa koki za maji, kuvunja masinki na kufanya uharibifu mkubwa kwa sababu tu wao si watu wa mpira wamekuja kwa kazi nyingine tofauti.

Ninavyojua mashabiki wenyewe wa mpira hawana mambo mengi, wanakuja na tiketi zao, wanaingia na kwenda kukaa sehemu ambazo wamezoea na kutazama soka.

Tena wengine hata kama ni wa timu mbili tofauti, lakini wanafahamiana na kusubiriana wakati wa kutoka ili kwenda nyumbani pamoja.

Lakini juzi, kuna taarifa kuwa watu wamekabwa na kuporwa pesa, mali na nyaraka zao tofauti tofauti, wakati matukio hayo yalikuwa yamepungua sana kama si kwisha kabisa, katika mechi ambazo watu wanaingia kwa pesa, hata zile ambazo mechi ziliziisha saa 6:00 usiku kama ile ya Kombe la Shirikisho, kati ya Simba dhidi ya US Gendamarie ya Niger iliyochezwa mwaka 2022, ambayo ilianza saa 4:00 usiku, hakukusikika hata kifo cha sisimizi.

Mashabiki wengine ambao walikata tiketi zao, baadhi wakitoka mikoani, walilazimika kuangalia mechi kwenye vibanda umiza na baa zilizo kando ya Uwanja wa Benajmin Mkapa, baada ya kukuta uwanja umejaa na hauruhusiwi tena mtu kuingia.

Yanga ilitangaza kuingia bure mashabiki upande wote wa mzunguko, huku kukiwa na upande mwingine ambao watu walitakiwa kulipa viingilio.

Mimi nadhani ifike wakati sasa, viongozi wa Yanga waachane na tabia hii, badala yake ipunguze viingilio, japo hata waingie kwa Sh. 2,000 tu, ili kuepuka madhara ambayo nimetoka kuyasema.

Serikali na Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), visikae kimya, kwani mchelea mwana kulia mwisho hulia mwenyewe, tusisubiri madhara makubwa yatokee ndipo hatua zichukuliwe ikiwamo kuunda tume.

Kuna viashiria kabisa vinaonekana kuwa huko mbele tunakokwenda kama hali hii itaendelea kuwa hivi kuna kitu kikubwa kinaweza kutokea, hivyo wakati wa kudhibiti ni sasa.

Mechi kubwa kama hizi ambazo kwa kawaida tu hata kwa kiingilio watu wanaweza kujaa, halafu inafanywa bure ni hatari sana.

HABARI KITAIFA

## Jafo aita wawekezaji nishati safi ya kupikia

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imetoa wito kwa mashirika na wadau mbalimbali wa mazingira kuwekeza katika nishati safi ya kupikia ili kurahisisha upatikanaji nishati hiyo kwa wananchi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki alipokutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi wa Shirika la UpEnergy Tanzania, Rehema Mbalamwezi katika Ofisi ya Makamu wa Rais jijini Dar es Salaam.

Katika mazungumzo hayo, waziri huyo alimpongeza mkurugenzi wa shirika hilo kwa kuunga mkono juhudi za serikali za kuhamasisha jamii kutumia nishati safi ya kupikia kwa lengo la kuhifadhi mazingira.

Dk. Jafo alisema mchango wa shirika hilo wa kuleta majiko yanayotumia nishati safi ya kupikia utasaidia kuhamasisha jamii kuachana na matumizi ya kuni na mkaa na kuanza kutumia nishati safi.

Kutokana na hatua hiyo, waziri huyo alishauri shirika hilo kutanua wigo wa uwekezaji wa nishati hiyo kwa kufungua matawi katika maeneo mbalimbali nchini ili wananchi wanufike na majiko hayo kwa urahisi na kwa bei nafuu.

Dk. Jafo pia alieleza nia ya serikali katika kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ambapo jambo hilo hivi sasa limeshika kasi likisimamiwa moja kwa moja na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Hivyo, alitaka wawekezaji hao kujitokeza kwa wingi katika kuunga mkono jitihada hizo za serikali katika kukabiliana na ukataji miti kwa ajili ya kuni na mkaa.

Mkurugenzi Mtendaji wa UpEnergy, Rehema, alieleza adhma ya kampuni hiyo katika kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi yanayoikabili nchi na dunia kwa ujumla.

Alisema shirika hilo limekuja na majiko banifu yanayotumia nishati safi ya umeme isiyozalisha gesi joto pamoja na majiko yanayotumia mkaa kidogo.

Takriban hekta 469,420 za misitu hupotea kila mwaka kwa shughuli za kibinadamu ikiwamo ukataji miti kwa ajili ya kuni na mkaa, hali inayosababisha uharibifu wa mazingira.

Inaelezwa kuwa wanawake ndio waathirika wakubwa wa matumizi ya nishati isiyo safi (kuni na mkaa), hali inayosababisha wakabiliwe na changamoto za kiafya kutokana na moshi unaotoka wakati wanafanya shughuli za upishi.

# Watoto 196 wapewa ujauzito

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

WATOTO wa kike 196 wamepewa ujauzito na wengine 69 kuolewa wilayani Iramba, mkoani Singida katika kipindi cha miezi 12 ya mwaka jana.

Ofisa Ustawi wa Jamii wilayani Iramba, Happiness Alex, alibainisha ukatili huo juzi katika kikao cha Kamati ya Ulinzi wa Mwanamke na Mtoto. Alex alisema kati ya watoto hao waliopewa ujauzito, 18 ni wanafunzi na watoto walio nje na taasisi ni 179.

Alisema kuwa matukio ya ulawiti kwa watoto wa kiume yanazidi kuongezika; kwa mwaka 2022 yalikuwa matano na 2023 yaliyoripotiwa 19, hali ambayo inaipa kamati kazi ya ziada kunusuru jamii.

Alex alisema sababu za kuongezeka kwa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto ni umaskini, mila na desturi kandamizi, matumizi mabaya ya utandawazi, mmomonyoko wa maadili na malezi hasi ya wazazi na walezi.

Mkuu wa Dawati la Jinsia la Jeshi la Polisi, Nduara Mbalamwezi alisema matukio yaliyoripotiwa polisi ni 82 kwa mwaka 2023. Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika kikao hicho, aliagiza wajumbe wa kamati hiyo kuwa makini na wageni wanaokuja wilayani mwao na ajenda mbalimbali ambazo hazina maadili kwa sababu ndio wanachochea vitendo hivyo.

"Mkiona mambo hayo yanafanyika, toeni taarifa kwenye mamlaka husika ili hatua zichukuliwe haraka kwa ajili ya kukomesha vitendo hivi ambavyo kimsingi vinawaathiri watoto ambao ni nguvukazi ya taifa baadaye," alisema.

Katiba ya Tanzania (1977), Sheria ya Ulinzi wa Mtoto (2009) na mikataba ya kimataifa ambayo nchi imeiridhia vinazuia ukatili wa kingono dhidi ya watoto.



Baadhi ya viongozi wa dini ya Kiislamu na Kikiristo wakichukua futari iliyoandaliwa na Taasisi ya Kilimanjaro Dialogue Institute (KDI) yenye makao yake makuu jijini Dar es Salaam inayojihusisha na Amani na Maridhiano ikiwa ni sehemu ya Mfungo wa Kwaresima na Mwezi Mtukufu wa Ramadhan yenye ujumbe wa "Sikukuu ya Amani" mwishoni mwa wiki. **PICHA: ASHAKI MIRAJI**

# Mtumbwi walipuka ziwani, wawili wahofiwa kufa maji

**Na Remmy Moka,** SAUT

WATU wawili wa familia moja, wakazi wa Majita, Wilaya ya Musoma Vijijini, mkoani Mara wanahofiwa kufariki dunia na wengine wawili kunusurika baada ya mtumbwi waliokuwa wanatumia katika shughuli za uvuvi kulipuka moto wakiwa Ziwa Victoria.

Wanaohofiwa kufa maji ni Lenard Masabali na Kasure Zacharia ambao walikuwa wanaendelea na shughuli zao za uvuvi ukiwa ni utaratibu wao wa kila siku kujitafutia riziki katika Kisiwa cha Gosba na Ukara ndani ya Ziwa Victoria.

Kwa mujibu wa mashuhuda wa tukio hilo, mtumbwi waliokuwa wanatumia ulilipuka na kuwaka moto baada ya mpira wa tangi la mafuta ya petroli kuchomoka na kusababisha mafuta kusambaa ndani ya mtumbwi huo.

Wakizungumza katika kambi ya kusubiri miili ya watu hao Mwalo wa Kinyang'wena, baadhi ya ndugu akiwamo Mariamu Paschal, walidai kuwa baada ya mafuta kusambaa ndani ya mtumbwi, wavuvi hao waliingiwa na hofu ndipo wakajirusha ndani ya maji ili kunusuru maisha yao.

Alidai kuwa baada ya wavuvi hao wanne kujirusha ndani ya maji mtumbwi ulilipuka na ni wawili pekee walioonekana hadi jana, jambo lililoibua taharuki na simanzi kwa wenyeji wa maeneo hayo kutokana na kutojua waliko wawili hao.

Shuhuda mwingine Fredrick Mussa alisema kuwa baada ya kuwakosa ndugu zao kama ulivyo utaratibu kwa mtu anayekufa maji, wameamua kuweka kambi katika mwalo huo ikiwa ni sehemu ya shughuli za msiba huku wakisubiri kama watapata miili yao wakazike.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kinyang'wena, Seleman Makanje alithibitisha kutokea tukio na kusema kuwa baada ya mafuta hayo kusambaa yalikutana na jiko la moto walilokuwa wakilitumia kupika ndani ya mtumbwi huo na kusababisha mlipuko huo. Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Mara, Augustine Magele, akielezea tukio hilo, alisema vijana hao waliingiwa na hofu wakati moto huo ulipoanza kusambaa, hivyo kuamua kujirusha ndani ya maji kwa lengo la kunusuru maisha yao.

Alisema kuwa kabla ya tukio hilo, mpira wa tangi la mafuta ulichomoka na kusababisha mafuta kusambaa ndani ya mtumbwi huo ndipo ukakutana na moto uliokuwa unawaka katika jiko la wavuvi hao.

Alisema jiko hilo lilikuwa linatumiwa na wavuvi hao kupika ndani ya mtumbwi wakati wa shughuli zao za uvuvi nyakati za usiku. Aliwasihi wavuvi wanaotumia mitumbwi inayotumia mafuta ya petroli au mafuta ya aina yoyote, kuacha kufanya shughuli zinazohusiana na kuwasha moto ndani ya mitumbwi hiyo ili kuepuka madhara kama hayo.

KABWELA Na Fadhili Mohammed



HABARI KITAIFA

# Mwalimu jela miaka 30 kunajisi mwanafunzi

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara imemhukumu kifungo cha miaka 30 gerezani Nestory Michael (23), mkazi wa wilaya ya Masasi ambaye ni mwalimu wa Shule ya Msingi Mkalapa wilayani Masasi kwa kosa la kunajisi mwanafunzi wake mwenye umri miaka 13.

Mwanafunzi huyo (jina linahifadhiwa) anasoma darasa la saba katika shule aliyokuwa anafundisha mwalimu huyo.

Akisoma hukumu hiyo mahakamani huko, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa mahakama hiyo, Batista Kashusha alisema mahakama imeridhika na ushahidi uliotolewa na upande wa Jamhuri ambao umethibitisha mashtaka dhidi ya mshtakiwa Michael pasipo shaka yoyote.

Hakimu Kashusha alidai mahakamani huko kwamba wakati wa usikilizwaji shauri hilo, upande wa Jamhuri ulikuwa na mashahidi saba na vielelezo.

Alisema kuwa kutokana na ushahidi uliotolewa na upande wa Jamhuri na mahakama kujiridhisha na ushahidi huo, inamtia hatiani mshtakiwa kwa kosa hilo la unajisi na kumhukumu kifungo cha miaka 30 gerezani.

"Ninamtia hatiani mshtakiwa katika shitaka hili la ubakaji baada ya upande wa Jamhuri kuthibitisha mashtaka dhidi ya mshtakiwa kwa kuleta mashahidi na vielelezo ikiwamo kielelezo cha daktari hivyo ninamhukumu kifungo cha miaka 30 jela," alisema hakimu Kashusha.

Hakimu Batista alisema hukumu hiyo imezingatia mambo yote ya msingi ya kisheria ikiwa ni pamoja na kubaini kuwa kweli tukio la ubakaji limetokea kwa kujiridhisha na vielelezo vya ushahidi uliotolewa na upande wa Jamhuri.

Awali Mwendesha Mashtaka Wilaya ya Masasi, Wakili wa Serikali Mwandamizi Miraji Kajieul aliiomba mahakama itoe adhabu kali dhidi ya mshtakiwa kutokana na kosa alilotenda.

Wakili huyo alidai kutolewa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa kutakuwa fundisho kwa watu wengine wenye nia ya kufanya vitendo kama hivyo vya unajisi.

Wakili Kajieul alidai mshtakiwa alitenda kosa hilo Septemba 26, 2023 katika maeneo ya shule hiyo ya Mkalapa majira ya mchana.

Mshtakiwa aliiomba mahakama hiyo kumpunguzia adhabu kwa kuwa yeye ni baba wa familia ya watoto wawili na mke mmoja na mama yake mzazi ambapo wote kwa pamoja wanamtegemea kimaisha.



Diwani wa Kata ya Songe,Wilaya ya Kilindi,Mkoa wa Tanga, Mohamed Makengwa (wanne kulia) akitoa maelezo kwa Ofisa Elimu Sekondari, Wilaya ya Kilindi, Ntuli Mwakabungu (wa tatu kulia) alipotembelea mradi wa ujenzi wa madarasa ya kidato cha nne na tano yanayojengwa Shule ya Sekondari Seuta kwa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 400. Wa pili kulia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi,Ally Mbwego na wengine ni wajumbe wa kamati hiyo. **PICHA: DEGE MASOLI**

# TANROADS yakusanya mamilioni faini za magari

**Na Said Hamdani,** LINDI

OFISI ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Lindi imekusanya Sh. 231,300,341 zilizotokana na ulipaji faini kutoka magari 939 yaliyokutwa kutokana na kosa la kuzidisha uzito unaotajwa kisheria.

Hayo yalibainishwa aliyekuwa Meneja wa TANROADS Mkoa huo, Robart Mosea kwenye kikao cha Bodi ya Barabara kilichofanyika ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa huo mjini Lindi.

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa amemwondoa Mosea katika nafasi ya meneja na kumrejesha makao makuu kupangiwa majukumu mengine kwa madai ya kushindwa kusimamia majukumu aliyokabidhiwa.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji, Mosea alisema makusanyo hayo ni ya kipindi cha miezi saba kuanzia mwezi Julai 2023 hadi Februari 2024, ambapo magari makubwa 138,716 yaliyotumia barabara kuu ya Kibiti-Lindi yalipimwa kupitia mizani zilizoko Nangurukuru, wilayani ya Kilwa na Mingoyo-Lindi.

Mosea alisema kati ya magari hayo, 56,099 sawa na asilimia 40.44 yalibainika kuongeza uzito unaokubalika kisheria na 939 sawa na asilimia 0.67 yalikutwa yamezidisha uzito zaidi ya asilimia tano inayoruhusiwa na kutozwa faini jumla ya Sh. 231,300,341.

"Hadi kufikia mwisho mwa mwezi Februari mwaka huu, fedha zote za faini zimelipwa," alisema Mosea na kueleza kuwa bajeti ndogo inayoidhinishiwa haikidhi matengenezo yanayohitajika katika barabara.

Mosea alisema TANROADS itaendelea kuweka vipaumbele maeneo korofi zinashughulikiwa kwa kadri ya upatikanaji fedha kuhakikisha zinapitika kwa nyakati zote na zile za msimu wa masika.

# CCM yamulika ufanisi utekelezaji wa miradi

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

HALMASHAURI Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Bagamoyo imeelekeza viongozi wa kata kusimamia miradi ya maendeleo na maeneo yenye kasoro yaainishwe ili wahusika wachukuliwe hatua.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Bagamoyo, Abdulsharifu Zahoro alielekeza hayo mwishoni mwa wiki baada ya mkutano wa Halmashauri Kuu ya chama hicho uliofanyika Chalinze, wilayani Bagamoyo.

Alisema wametoa maelekezo kwa watendaji hao wa kata wazingatie kusimamia kwa karibu miradi hiyo ili itekelezwe kulingana na fedha zilizotolewa.

Zahoro pia alionya tabia ya baadhi ya wanachama wanaojiita "chawa", kugombanisha viongozi na wanachama; wanatakiwa kuwaacha viongozi wafanye kazi zao kwa malengo waliyojiwekea.

"Tuache kuunda maneno kwa viongozi, kiongozi aliyeko madarakani atapimwa kwa kazi anazofanya, na hiki si chama cha chawa, msitugombanishe na msiwagombanishe viongozi wenu na wanachama," alionya.

Mwenyekiti huyo pia aliekeza kila kiongozi aliyetoa ahadi anatakiwa kuitekeleza mapema ili kuepuka vikwazo ambavyo vinaweza kutokea kipindi cha uchaguzi.

Vilevile, alitumia muda huo kuonya baadhi ya wanachama walioanza kujipitisha kwenye maeneo mbalimbali wakionesha nia yao ya kutaka kugombea nafasi za uongozi, akiwataka kuacha mara moja kufanya hivyo hadi pale muda utakapofika.

"Muda ukifika kila anayetaka achukue fomu kusiwe na ubaguzi lakini mkumbuke kuna viongozi wamefanya kazi sana katika wilaya hii," alisema.

Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Pwani, Subira Mgalu alisema wamekubaliana kuendelea kusimama na serikali kwa kufuatilia miradi mbalimbali inayotekelezwa na kufanya kazi kwa bidii, kuaminiana, kushirikiana na kuhakikisha ilani inatekelezwa.





# DC atoa onyo wafugaji wanaokata mabomba ya maji

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

MKUU wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Dk. Suleiman Serera, amewaonya baadhi ya wafugaji wanaokula njama ya kuharibu miundombinu inayotumika kusambaza maji katika jamii, ikiwamo kukata mabomba ya maji, kwa ajili ya kunywesha maji mifugo yao.

Alitoa onyo hilo juzi alipokuwa akizungumza na wananchi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Orkesumet.

Dk. Serera alilazimika kuwaonya wafugaji hao ili kunusuru mradi wa kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini, unaotekelezwa kwa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP).

Aidha, alisema siyo jambo la kufurahisha kuona baadhi ya wafugaji wanahusika kuhujumu miundombinu ya maji kwa kukata mabomba kwa kutumia silaha za jadi aina ya sime ili kupata ya kunywesha mifugo maji kwenye maeneo yasiyokuwa rasmi. "Serikali imetumia fedha nyingi kuwafikishia huduma ya maji mahali mlipo, hivyo tunzeni miundombinu ili iwe faida kwenu na kizazi kijacho," alisema Dk.Serera.

Hata hivyo, alisema ameshatoa maelekezo kwa vyombo vya ulinzi na usalama kushirikiana na jamii kuwabaini wahusika ili kuwachukulia hatua kali za kisheria wahusika.

Meneja wa Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) wa wilaya hiyo, Joanes Martin, alisema mradi huo utaboresha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wa eneo hilo.

Vilevile alisema upatikanaji maji katika Wilaya ya Simanjiro umefikia asilimia 66.7 na mradi huo utakuwa wa ubia kati ya serikali na sekta binafsi.

Ofisa wa RUWASA kutoka makao makuu, Emmanuel Burton, akizungumzia mradi huo, alisema utawanufaisha wananchi katika mikoa mitano ya Manyara, Lindi, Morogoro, Dodoma na Kagera pamoja na wilaya nyingine 15.

Pamoja na mambo mengine, alisema kwa Mkoa wa Manyara, wilaya zitakazonufaika na mradi huo alizitaja ni Simanjiro, Kiteto na Mbulu.



Waamini wa kanisa la Anglikana mtaa wa Madaba wilayani Muheza Tanga wakiwa katika maandamano ya kuingia kanisani hapo jana ambayo yaliongozwa na Mchungaji wa kanisa hilo, Paul Luhinga katika Ibada ya Sikukuu ya kufufuka kwa Yesu Kristo maarufu Pasaka. **PICHA:STEVEN WILLIAM**

# WWF, UCRT wapewa tahadhari upimaji ardhi

**Tumaini Mafie,** LONGIDO

SERIKALI imeyatahadharisha mashirika ya World Wide Fund (WWF) na Ujamaa Community Resource Team (UCRT), kutoingia katika Wilaya ya Longido, mkoani Arusha na mpango wa upimaji wa ardhi yao ili kutekeleza miradi ya uhifadhi jumuishi wa mazingira na kuboresha maisha ya jamii.

Wameelezwa kuwa kwa kufanya hivyo kutaongeza zaidi migogoro ya ardhi.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Marco Ng'umbi alitoa onyo hilo juzi alipokwenda kuzindua mradi huo unaolenga kuwanufaisha wafugaji wa jamii ya kimasai wa wilaya mbili za Longido na Ngorongoro, kupitia mradi wa uhifadhi shirikishi unaojumuisha binadamu na wanyama.

"Kwa bahati nzuri wilaya hii ina vijiji 49 na vyote vina ramani na vimepimwa. Hatutegemei UCRT, WWF na wengine kuja kuweka mipaka mipya.

"Mkijaribu kufanya hivyo ni kutengeneza migogoro ya ardhi. Mnachotakiwa kufanya ni kusaidia kupanga vizuri matumizi sahihi ya kila kipande cha ardhi." alisema.

Mratibu wa UCRT wa Wilaya ya Longido, Jamboi Baramayesu, alisema mradi huo unagharimu Dola za Marekani milioni 1.488, sawa na zaidi ya Sh. bilioni tatu.

Kwa mujibu wa Baramayesu, mradi huo unatarajia kuvinufaisha vijiji 10 vya Wilaya za Longido na Ngorongoro.

Zaidia alifafanua: "Mradi huu unahudumia klasta tatu, ambazo ni klasta ya Ziwa Natron na Longido Magharibi, na klasta ya pili ni ya Ziwa Eyasi na Bonde la Yaeda, wakati ya tatu ni Simanjiro na Kiteto.

Kwa klasta ya Ziwa Natron na Longido Magharibi, vijiji vinavyopitiwa na mradi ni 10, kwa maana ya Ngorongoro vinne na Longido, vijiji sita."

Baadhi ya wananchi wakizungumza kuhusu mradi huo akiwemo Richard Mollel alisema mradi huo ni rafiki kwao na ni moja ya aina ya mradi unaotakiwa katika jamii ya kifugaji kutokana na kuwa shirikishi na unaojumuisha binadamu na wanyama.

Mkazi mwingine, Hellena John, alisema mradi huo unawapa fursa ya kushiriki katika kuhifadhi na vyanzo vya maji, ambavyo vimekuwa vikivamiwa kwa namna moja ama nyingine kutokana na kutokuwepo kwa mipaka thabiti.

## Kaya 59,904 zapewa bil.2.5/- kujikwamua umasikini

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MPANGO wa Kunusuru Kaya Masikini, unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), umezinasua kwenye ufukara kaya 59,904 zilizoko katika Mkoa wa Arusha, baada ya kuziwapatia ruzuku ya zaidi ya Sh. bilioni 2.5

Kaya hizo ambazo ni sawa na walengwa 62,667 wa mpango huo walioko katika vijiji na mitaa 577, walipewa ruzuku hiyo ya uhawilishaji fedha katika dirisha la miezi ya Novemba na Desemba mwaka jana.

Mratibu wa TASAF Mkoa wa Arusha, Richard Nkini, alisema mgawanyo wa fedha hizo, umezingatia kaya zilizoko kwenye mpango kwa kila halmashauri.

Mratibu huyo, alitaja na kuweka wazi mgawanyo huo kuwa Sh. milioni 551.6 zimegawiwa kwa kaya 13,795 za Halmashuri ya Arusha, Sh. milioni 174.6 kwa kaya 4,385 za Halmashauri ya Jiji la Arusha na Sh. milioni 328.9 kwa kaya 7,761 kwa Halmashauri ya Karatu.

Pia, alisema Sh. milioni 318 kwa kaya 7,177 katika Halmashauri ya Monduli, Sh. milioni 447.1 kwa kaya 10,111 kwa Halmashauri ya Ngorongoro, Sh. milioni 301.6 kwa kaya 7,769 kwa Halmashauri ya Meru, huku Sh. milioni 388.9 zikigawiwa kwa kaya 8,905 za Halmashauri ya Longido.

Hata hivyo, alisema lengo la serikali la kuhawilisha fedha hizo ni kuziwezesha kaya hizo kujiinua kiuchumi na kijamii, kupitia miradi mbalimbali inayotekelezwa na TASAF pamoja mradi wa kuweka akiba kupitia vikundi vya kuweka, kuwekeza na kukopa

Vilevile, alisema TASAF ni mpango wa serikali unaolenga kusaidia kaya masikini nchini, kupitia uhawilishaji fedha moja kwa moja kwa walengwa.

Lengo ni kuinua hali ya maisha ya kaya zilizoko katika mazingira hatarishi na kuhakikisha kaya hizo, zinatumia fedha kulingana na ruzuku zilizoainishwa za msingi, elimu na afya.

Alisema: "Mpango wa TASAF ni jitihada za serikali za kupunguza umaskini na kukuza maendeleo ya jamii na kupitia programu ya kutoa fedha moja kwa moja kwa walengwa ili kuongeza upatikanaji wa huduma za msingi kama elimu na afya pamoja na kuboresha uwezo wa kaya hizo kujikimu kiuchumi".

Alisema programu hiyo imekuwa na matokeo chanya kwa walengwa katika kupunguza umaskini uliokithiri na kuongeza ustawi wa jamii nchini, kupitia tathmini ambayo hufanywa kwa kina na kuhakikisha kuwa misaada inawafikia walengwa kwa usahihi.





# Wajasiriamali walia ukosefu mashine, waiangukia serikali

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

WAJASIRIAMALI waliofungua kiwanda kidogo cha kutengeneza bidhaa zitokanazo na ngozi Kiloleli wilayani Kishapu, wamesema ukosefu wa mashine ni mojawapo ya kikwazo katika utekelezaji wa shughuli zao.

Hivyo, wameiomba serikali kuwafadhili ili kujikwamua kiuchumi.

Walitoa ombi hilo juzi kiwandani hapo zinapotengenezwa bidhaa za ngozi vikiwamo viatu, mikanda na mikoba ili kuondokana na adha ya kufuata malighafi ya ngozi jijini Mwanza na kuanza kuzichakata wenyewe.

Mmoja wa wajasiriamali hao, Joseph Soleya, alisema endapo watafanikiwa kupata mashine hiyo itawanufaisha pia wafugaji wilayani hapa kupitia ngozi za mifugo yao na kuinuka kiuchumi wao na kuchangia Pato la Taifa.

"Hapa wapo ng'ombe wengi, hivyo tukiwa na mashine yetu sisi wenyewe ya kuchakata ngozi itaongeza thamani ya mifugo, hivyo ombi letu kwa serikali itufadhili mashine hiyo,"alisema Soleya.

Makamu Mwenyekiti wa kikundi hicho, Rejina Emmanuel, alisema kilianzishwa mwaka 2019 na kina wanachama 17, wanawake 10 na wanaume saba, kikilenga kukuza uchumi wa kila mwanachama na kutoa huduma kwa jamii.

Alisema licha ya serikali kuwapatia elimu ya kukabiliana na mazingira lakini bado haitoshi, hivyo iendelee kutoa elimu kwa kila mwana jamii ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira na kuongeza ubunifu kwa wajasiriamali hapa nchini.

Katibu Msaidizi wa Kituo cha Taarifa na Maarifa kupitia (TGNP) Kiloleli wilayani Kishapu, Zacharia Pimbi, alisema elimu ya ubunifu na namna ya kuibua miradi, iliwawezesha wajasiriamali hao kupata fursa ya kuanzisha kiwanda kidogo cha kutengeneza bidhaa hizo.

Alisema kiwanda hicho kinatakiwa kuwa msaada kwa jamii ya wafugaji kijijini hapo kutokana na kuwepo kwa mifugo mingi na wajasiriamali wengi ambao wanaitaji elimu stahiki ili kujiendeleza kiuchumi.

Kikundi hicho kiliwezeshwa Sh.milioni 95.6 kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kupitia mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi vijijini, huku Halmashauri ya Kishapu ikiwapa asilimia 10 sawa na Sh.milioni 10 ili kuongeza wigo wa mitaji yao katika shughuli zao za uchakataji wa malighafi ya ngozi.

# PAC kufuatilia mabilioni Mradi wa Maji Ziwa Victoria

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imesema itakutana na Katibu Mkuu Wizara ya Maji, ili kuona Sh. bilioni 24 za utekelezaji wa Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria kutoka Tinde wilayani Shinyanga hadi Shelui Singida, kama zimefikia lengo lililokusudiwa na kutoa huduma stahiki kwa jamii.

Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Japhet Hasunga alibainisha hayo juzi wakati walipotembelea tangi la mradi huo lililopo Kijiji cha Buchama, Kata ya Tinde wilayani Shinyanga lenye ujazo wa lita 1,150,000.

"Kuna taarifa kwamba vijiji vingine bado havina maji kikiwemo kijiji lilipo tangi kuu, hivyo tutakwenda kupata majibu vizuri kutoka wizarani na kufuatilia Sh. bilioni 24 namna zilivyotumika ili kuona kama malengo yamefikiwa" alisema Hasunga.

Alisema kazi ya kamati hiyo ni kufuatilia fedha ambazo zimetolewa na serikali na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya wananchi.

Hivyo baada ya kuona mradi huo na upungufu wake alisema, watakutana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, ili kuona fedha hizo endapo zimefanya yale yaliyotakiwa na kufikia lengo lililokusudiwa.

Mjumbe wa kamati hiyo, Ravia Faina, alisikitishwa kusikia Kijiji cha Buchama ambacho limejengwa tangi hilo hakina huduma ya maji na kuishauri serikali iwapatie maji haraka kwani wao ndiyo walinzi wakuu wa mradi huo.

Awali akitoa taarifa ya mradi huo, Tito Alex kutoka Wizara ya Maji, alisema umekamilika kwa awamu ya kwanza.



Wajasiriamali kutoka Kikundi cha Kalangale Kata ya Kiloleli wilayani Kishapu, juzi wakiwa kwenye kiwanda chao kidogo cha kutengeneza bidhaa mbalimbali zitokanazo na ngozi, wakionyesha baadhi ya bidhaa hizo vikiwamo viatu, mikanda na mikoba huku kilio chao kikuu ikiwa ni ukosefu wa mashine yao wenyewe ya kuchakata ngozi ili wapate maligafi hapo hapo kiwandani kwao na kuongeza thamani ya mifugo wilayani Kishapu, na siyo kufuata ngozi Jijini Mwanza na kuingia gharama kubwa.
**PICHA: MARCO MADUHU**

# Wakuu wa shule waagizwa kuanzisha kilimo cha chakula

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KAMATI ya Elimu, Afya na Maji ya Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga imewataka walimu wakuu pamoja na wakuu wa shule kutumia maeneo ya shule wanazozisimamia kuanzisha kilimo cha mazao ya chakula.

Hatua hiyo inatajwa kuwa mwarobaini wa tatizo la utoro shuleni, ufaulu hafifu pamoja na michango inayotolewa na wazazi kwa ajili ya kulipia chakula shuleni.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Mwenyakiti wa Kamati hiyo, Doa Limbu katika kikao cha tathimini ya mitihani na matokeo ya kidato cha nne na darasa la saba na kutaja hali hiyo kuwa itapandisha kiwango cha ufaulu.

Alisema shule za msingi na sekondari zilizopo zinamaeneo makubwa ambayo wameyaacha na kuwa vichaka, ilihali wakiyatumia yatakuwa msaada mkubwa katika kuzalisha chakula kwa ajili ya wanafunzi na kuondoa michango kwa wazazi.

"Malalamiko yasiyokuwa ya msingi kutoka kwa wazazi yamekuwa mengi, hivyo mkijikita katika shughuli za kilimo itakuwa si tu msaada katika kuinua ufaulu bali pia kuondoa mivutano na wazazi," alisema.

Aliongeza: "Tunahitaji kuongeza ufaulu wa wanafunzi kutoka asilimia 80 kwa wanafunzi wa darasa la nne na asilimia 71 kwa darasa la saba na hii inawezekana pale wanafunzi watakapokuwa wanapata chakula shuleni, kwamba chakula kinapatikana kutoka kwa wazazi na kuanzisha kilimo kwenye maeneo yetu ya utawala," alisisitiza Limbu.

Ofisa Elimu Taaluma wa Halmashauri hiyo, Silivanus Bonda alisema suala la chakula shuleni ni wazazi, walezi na bodi za shule katika kupanga viwango vya chakula kwa kila mwanafunzi.

Alisema kuanzishwa kwa mashamba hayo itasaidia kuondokana na michango hiyo kwakuwa chakula kitakuwa kikizalishwa na wanafunzi wenyewe.

Mkurugenzi wa Ushetu, Hadija Kabojela aliwataka walimu hao kushughulikia tatizo la utoro ambalo ni chanzo cha kutokufanya vema kwenye mitihani ya mwisho ya darasa la nne na saba ili kuongeza ufaulu kutoka asilimia 80 iliyopo kwa sasa hadi kufikia asilimia 100 ya lengo lililokusudiwa.

Nipashe
Spotika



CARLOS TEVEZ 12 - 13



# MCHEZAJI MMOJA TIMU SITA EPL ANAYEPASWA KUUZWA

**LONDON,** England

BADO kuna mpira mwingi wa kucheza msimu wa 2023/24, lakini ikiwa timu hazitazamii dirisha la usajili la majira ya joto na msimu ujao tayari zimeshindwa.

90min inawaangalia mchezaji mmoja kutoka kwenye kila timu sita kubwa - Arsenal, Chelsea, Liverpool, Manchester City, Manchester United na Tottenham Hotspur - ambao wanapaswa kuuzwa mwishoni mwa msimu huu, twende sasa...

**Arsenal: Aaron Ramsdale**

Aaron Ramsdale kuendelea kuwa kwenye benchi la Arsenal haitamsaidii, na kwa chaguo la kudumu la pauni milioni 27 katika mkopo wa David Raya kutoka Brentford haitabadilisha lolote.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, alichaguliwa katika Kikosi Bora cha Mwaka cha Ligi Kuu England kwa msimu wa 2022/23, lakini ameona nafasi yake ya kuwa namba moja wa England kwenye Euro 2024, ambayo ilikuwa uwezekano wa kweli miezi 12 iliyopita, imepotea. Arsenal wana deni kwake kusikiliza ofa na pengine wanaweza kuamuru ada ya ziada ya pauni milioni 30 ambayo walikubaliana na Sheffield United mnamo 2021.

**Chelsea: Marc Cucurella**

Chelsea hawajapata lolote kutokana na uwekezaji wao kwa viungo wa kati Moises Caicedo na Enzo Fernandez (pauni milioni 223 kwa ajili ya wawili hao), hivyo wanaweza pia kuwavumilia kutokana na kwamba wote wawili bado wako katika hatua za awali za maisha yao ya soka na bado wanaweza kuja vizuri baada ya muda.

Marc Cucurella hakupaswa kusajiliwa kwa kikosi cha kwanza na kurejesha fedha nyingi zaidi ni rahisi kuliko kama Mykhailo Mudryk au Wesley Fofana, wote wawili walio na bei kubwa zaidi, wanaweza kuuzwa katika siku za usoni. Crystal Palace, West Ham, Brentford, au hata kurejea Brighton - wakitoa chochote cha karibu pauni milioni 30, Chelsea wanapaswa kuchukua.

**Liverpool: Cody Gakpo**

Cody Gakpo amekuwa Liverpool kwa zaidi ya mwaka mmoja tu, lakini Mholanzi huyo hana jukumu lililobainishwa na kwa njia yoyote unayoitazama hana nafasi katika kikosi cha kwanza. Katika nafasi yake ya kwanza mbele, ushindani kutoka kwa Darwin Nunez, ambaye Liverpool umeongezeka kutokana na kiwango kikubwa cha raia huyo wa Uruguay msimu huu.

Kwa namna Diogo Jota alivyo ndiye anayeweza kusema kuwa ni namba tisa, na kumuacha Gakpo katika hali ya kutatanisha. Pauni milioni 37 iliyolipwa, ambayo inaweza kufanyika kwa kuzingatia umri wake na uwezo wake uliobaki, inaweza kuwa uamuzi wa busara.

**Manchester City: Bernardo Silva**

Je, unatafuta nani kuendelea wakati wewe ni timu bora zaidi duniani na kila mtu anaonekana kufurahishwa na hali yake? Jibu ni gumu sana.

Labda ni wakati wa kumpa Bernardo Silva matakwa yake na kumwacha aende. Licha ya kusalia kuwa mmoja wa wachezaji muhimu wa Pep Guardiola, Mreno huyo hajatulia nje ya uwanja tangu 2020 na katika umri wake wa miaka 29 hadi Agosti, bado anaweza kuwa na bei kubwa.

Mara kwa mara, City wana mazoea ya kuwaruhusu wachezaji muhimu kuondoka kama ilivyokuwa kwa Raheem Sterling, Joao Cancelo, Gabriel Jesus - na nafasi zao kuchukua vijana - Jeremy Doku, Josko Gvardiol na Erling Haaland.

**Manchester United: Antony**

United ilimfanya Antony kuwa mchezaji wa pili ghali zaidi katika historia yake wakati uhamisho wa pauni milioni 86 kutoka Ajax ulipotiwa saini mwaka 2022, huku maskauti wakiwa wamemtathmini winga huyo hapo awali kama mchezaji wa pauni milioni 25.

Mbrazil huyo alianza vema, akifunga katika kila mechi tatu za kwanza za Ligi Kuu England na baadaye akapata bao lililoiondoa Barcelona kwenye Ligi ya Europa. Lakini kiwango chake kilipotea miezi mingi kabla ya matatizo ya nje ya uwanja.

Hivyo United ili isipate hasara inaweza kumuuza ili kutafuta kwingine.


**Tottenham Hotspur: Tanguy Ndombele**

Huku mkataba wake ukitarajiwa kukamilika mwaka 2025, msimu huu wa kiangazi ndio nafasi ya mwisho kwa Tottenham Hotspur kuweza kumtoa Tanguy Ndombele kwa ada yoyote ya uhamisho, baada ya kukubali dili la rekodi ya klabu yenye thamani ya pauni milioni 64.5 mwaka 2019. Kiungo huyo hajacheza hata kidogo kwa Spurs kwa zaidi ya miaka miwili tangu Januari 2022.

Galatasaray hawana uwezekano wa kutumia chaguo lao katika makubaliano yao ya mkopo yenye thamani ya chini ya pauni milioni 13 kutokana na kwamba bado hajaanza msimu huu. Kwa hiyo inaweza kuwa kesi ya kukubali hata kiasi cha kawaida ili tu kuondoa mzigo wa mwaka mwingine kwenye vitabu.

## ISIKUPITE

TANGU kuanza kwa hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu hadi sasa ikiwa ni hatua ya robo fainali, Klabu ya Petro de Luanda ya Angola ndiyo timu pekee ambayo haijapoteza wala kuruhusu bao (clean Sheet) langoni mwake.



# WACHEZAJI 6 WANAOWANIA UCHEZAJI BORA EPL 2023-24




RICE

**LONDON,** England

KAMPENI ya Ligi Kuu England ya 2023-24 imekuwa ya aina yake. Arsenal, Liverpool na Manchester City zote zipo katika vita ya farassi watatu kuwania taji la Ligi Kuu England. Ni wachezaji wachache tu ambao wameweza kutwaa tuzo ya mchezaji bora wa msimu mara mbili katika maisha yao ya soka kwenye ligi hiyo.

Orodha ya wachezaji hao ni pamoja na Thierry Henry, Cristiano Ronaldo, Nemanja Vidic na Kevin De Bruyne, na Ronaldo pekee ndiye aliyeshinda katika miaka miwili mfululizo (2007 na 2008).

Huku msimu wa Ligi Kuu ya 2023-24 ukielekea mwishoni, hebu tuwatazame wachezaji sita wanaowania taji la mchezaji bora wa msimu huu...

**#6. Mohamed Salah (Liverpool)**

Mchezaji bora wa msimu wa 2017-18 atalenga kuongeza taji la pili la Ligi Kuu na tuzo binafsi kwa mara ya pili.

Salah bado ana mabao 15 na asisti tisa katika mechi 22 alizocheza hadi sasa kabla ya mechi za wikendi.

Raia huyo wa Misri atakuwa akiwania Kiatu cha Dhahabu ambacho ni cha nne kwa rekodi katika Ligi Kuu England huku akiwa amefunga mabao matatu nyuma ya kiongozi wa ligi hiyo, Erling Haaland. Salah angeorodheshwa juu zaidi kama asingekuwa majeruhi baada ya kupata jeraha wakati wa Kombe la Mataifa ya Afrika nchini Ivory Coast mapema mwaka huu.

Hakuna shaka kuwa Salah ni mmoja wa wachezaji bora kuwahi kuichezea Liverpool. Lakini ikiwa anaweza kuiongoza Liverpool kutwaa taji lingine la ligi pamoja na tuzo ya pili ya mchezaji bora, atakuwa kwenye daraja la juu kama mmoja wa wachezaji bora wa wakati wote wa Ligi Kuu England.

**#5. Erling Haaland (Manchester City)**

Haaland alikuwa na nafasi nzuri ya kurudia kutwaa tuzo ya mchezaji bora kutoka msimu uliopita ambapo alitwaa na ingekuwa ni kwa mara ya pili mfululizo. Kwa bahati mbaya, jeraha lilimuweka nje kwa karibu miezi miwili na kuruhusu wengine kuchukua kasi.

Lakini raia huyo wa Norway bado anawindwa sana na tuzo nyingine ya mchezaji bora wa msimu huku akikaa kileleni kwenye mbio za Kiatu cha Dhahabu akiwa amefunga mabao 18 na asisti tano katika michezo 23 ya Ligi Kuu.

Haaland alikuwa mchezaji wa kwanza katika historia ya Ligi Kuu England kushinda tuzo ya mchezaji bora wa msimu na mchezaji bora chipukizi katika kampeni msimu uliopita.

Kwa wakati huu, kila mtu anakosa uwezo wa kumuelezea fowadi huyo wa Manchester City. Huku City wakikimbia kuwania taji lao la nne mfululizo la Ligi Kuu, watamtegemea Haaland na mabao yake kuwafikisha mbali zaidi.

**#4. Ollie Watkins (Aston Villa)**

Umekuwa msimu wa aina yake kwa Ollie Watkins na Aston Villa huku wakiendelea kupigania nafasi ya kuingia kwenye nafasi nne za juu za Ligi Kuu England. Villa chini ya kocha Emery Unai wameingia msimu huu wakiwa na ustadi wa juu, mpangilio na uchezaji bora, wakiongozwa na Watkins.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, kwa sasa anashika nafasi ya pili katika kinyang'anyiro cha Kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu ya England akiwa amefunga mabao 16 na ana pasi 10 za mabao. Akiwa anaongoza kwenye mchango wa mabao 26 kwa jina lake kwenye ligi, Watkins amekuwa chanzo cha mabao ya Villa msimu huu.

Villa wameshindwa katika michezo ya hivi karibuni. Lakini tunapokaribia mwisho wa msimu, watategemea kiwango cha ufungaji mabao ili kuwaongoza kupata nafasi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

**#3. Declan Rice (Arsenal)**

Rekodi ya kusajiliwa Arsenal ya pauni milioni 105 imekuwa yenye thamani ya kila senti moja hadi sasa. Baada ya kuyumba katika mechi 10 za mwisho za ligi msimu uliopita, Declan Rice amewapa 'Washikabunduki' uongozi unaohitajika na uimara wa ulinzi.

Kiungo huyo wa kati wa safu ya ulinzi hana kifani linapokuja

fanikiwa kufunga mabao sita ya msimu mmoja na kutoa pasi tano za mabao.

Rice amecheza katika kila mechi ya ligi msimu huu na ataendelea kufanya hivyo kwani Arsenal itakuwa ikitafuta taji lao la kwanza la ligi baada ya miaka 20. Iwapo Arsenal watalitwaa taji hilo Rice atakuwa mmoja wa washindani wa tuzo ya mchezaji bora wa msimu.

**#2. Phil Foden (Manchester City)**

Ni wachache sana wanaoweza kubishana na Pep Guardiola wakati kocha wa Manchester City aliposema Phil Foden ndiye mchezaji bora wa Ligi Kuu England baada ya mabao yake mawili dhidi ya Manchester United. Nyota huyo amebarikiwa kuwa na kipaji cha ubunifu, ambaye anaonekana kuwa mchezaji kamili akiwa na umri wa miaka 23 pekee.

Ni bidhaa ya akademi ya Man City tayari ina msimu wake bora mbele ya goli akiwa amefunga mabao 11 katika michezo 28 ya ligi na asisti saba kwa jina lake.

Uchezaji wake katika miezi ya hivi karibuni umemsukuma hadi namba mbili katika viwango. Ikiwa ataendelea hivyo, atakuwa mchezaji wa kwanza wa England kushinda tuzo ya mchezaji bora wa msimu tangu Jamie Vardy mnamo 2016.

**#1. Rodri (Manchester City)**

Rodri ameendelea kuwa katika kiwango kizuri. Mchezaji wa tatu wa Manchester City katika orodha hii, lakini bila shaka ndiye aliye muhimu zaidi kwa timu hiyo - Rodrigo anatoa homchango wa hali ya juu na kuwa kiungo bora zaidi wa ulinzi duniani, achilia mbali Ligi Kuu England. Kiungo huyo wa ulinzi anaongoza ligi akiwa na pasi nyingi zaidi (2634) na miguso (2989).

Man City wanacheza kwa kasi anayocheza Rodri kwani mara nyingi inaonekana wanatatizika anapokosekana. Wakati Haaland, De Bruyne na Foden wakinyakua vichwa vyote vya habari, ni Rodri ndiye anayeichezesha timu nzima.

Raia huyo wa Hispania amekuwa na ufanisi katika nafasi ya tatu ya mwisho akiwa na mabao sita na asisti tano katika jumla ya mabao yake. Anaweza kutegemewa kila wakati na mara nyingi huja na bao katika mechi kali zaidi. Kwa vile wachezaji bora kama Haaland na Salah wamekosa mechi chache msimu huu, Rodri ana nafasi nyingi ya kubeba tuzo ya mchezaji bora wa msimu huu.

## Nukuu


"Nasema hakujawa na mchezaji aliyepigwa mateke mengi kwenye Ligi Kuu kuliko Bukayo Saka. Tusipokuwa makini, soka litampoteza Bukayo akiwa na umri wa miaka 24 au 25 kwa sababu Saka atakuwa ameondolewa mchezoni. Nina uhakika kila mwamuzi atajaribu kulinda mchezo na mtu binafsi kwa njia bora zaidi," **Nguli wa Arsenal, Bob Wilson, akitaka marefa wamlinde Bukayo Saka kutokana na rafu nyingi anazochezewa.**



"Cristiano [Ronaldo] ni tofauti kabisa na Messi. Leo [Messi] alipokuwa anaanza, hakugusa ukumbi wa mazoezi [gym]. Lakini Cristiano alikuwa huko asubuhi, alasiri na jioni, wakati wote. Cristiano ilibidi afanye kazi na kujiandaa kuwa bora, wakati kwa Leo ni asili. "Hizo ndizo tofauti kubwa ambazo naona kati ya wachezaji wawili bora kwenye sayari. Messi anacheza mchezo mwingine. Kwa Messi kufunga mabao matatu [katika mchezo wowote] ni jambo la kawaida," **Carlos Tevez alipoangazia 'tofauti kubwa zaidi' kati ya Cristiano Ronaldo na Lionel Messi**



"Naweza kusema kwamba timu nyingine ninayoipenda zaidi ni Barcelona. Ninahisi kwamba wana mawazo na maadili sawa na Liverpool. Wanapenda kuleta wachezaji kupitia akademi. Nilikua nikimwangalia (Lionel) Messi na timu hiyo maalum ya Barcelona akiwa na (Andres) Iniesta, Xavi (Hernandez), (Thierry) Henry na (Samuel) Eto'o," **Beki wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold, kuhusu timu anayoipenda wakati huu pia akihusishwa kutakiwa na Real Madrid.**






Straika wa Yanga, Clement Mzize, akiwa ameruka juu kupiga mpira kichwa, akisababisha hatari kwenye lango la Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, akichungwa na beki Mosa Lebusa katika mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, iliyochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na kumalizika kwa sare tasa. **MPIGAPICHA WETU**

# YANGA ILIVYOLINDA REKODI CAF, YA SIMBA IKIVUNJWA

**Na Adam Fungamwango**

MECHI za kwanza za robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika zilimalizika kwa wawakilishi wa Tanzania, Simba kuchapwa bao 1-0 Ijumaa iliyopita katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, dhidi ya Al Ahly ya Misri, na Jumamosi Yanga kutoka suluhu dhidi ya Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini.

Majaliwa ya timu za Tanzania yapo kwenye mechi za marudiano zitakazochezwa Ijumaa wiki hii, Simba itakapokuwa nchini Misri na Yanga nchini Afrika Kusini ili kujua kama zote mbili au walau moja inaweza kutinga hatua ya nusu fainali.

Kipigo cha bao 1-0 ilichokipata Simba kimehitimisha rekodi nzuri ya timu hiyo kila inapocheza na Al Ahly hapa nchini.

Kwa mara ya kwanza Al Ahly imepata ushindi dhidi ya Simba nchini tangu timu hizo zilipoanza kukutana mara ya kwanza mwaka 1985.

Al Ahly imefanikiwa kuifunga Simba baada ya kucheza mechi nne bila mafanikio kwenye michuano mbalimbali ya kimafataifa hapa nchini.

Simba imeshinda mara tatu na sare moja, kabla ya kupoteza mechi ya Ijumaa, ikiwa ni mchezo wa tano timu hizo kukutana jijini Dar es Salaam.

Kwa upande wa Yanga imefanikiwa kulinda rekodi yake ya mwaka 2001 ya kutoka sare dhidi ya Mamelodi Sundowns. Hii ni mara ya pili timu hizo kukutana nchini na mara zote Yanga imepambana kuhakikisha haipoteza nyumbani.

Katika makala haya tumekusanya rekodi zote za timu hizo zilipochezwa nchini, Simba dhidi ya Al Ahly na Yanga dhidi ya Mamelodi Sundowns na matokeo yake hadi mechi za wiki hii, twende sasa...

**Simba 2-1 Al Ahly (1985)**

Mara ya kwanza Simba ilianza kucheza na Al Ahly, Agosti 22, 1985 kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza, ikiwa ni michuano ya Kombe la Washindi Barani Afrika, sasa Shirikisho, ikishinda mabao 2-1 yaliyofungwa na Zamoyoni Mogella na Mtemi Ramadhani, huku bao la kufutia machozi la Al Ahly likifungwa na Mohamed Ae Khatib 'Bibo' ambaye kwa sasa ndiye rais wa klabu hiyo.

**Simba 1-0 Al Ahly (2019)**

Ilikuwa ni Februari 12, 2019 mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi iliposhinda bao 1-0, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Baada ya kupigwa mabao 5-0, Februari 2 nchini Misri, Simba ilirejea nyumbani na kulipa kisasi hicho kwa bao lililowekwa wavuni na straika, Meddie Kagere. Simba na Al Ahly zote zilisonga mbele kwenye kundi hili.

**Simba 1-0 Al Ahly (2021)**

Timu hizo zilipangwa tena kwenye makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, 2021, na mechi ya kwanza ilicheza nchini kama kawaida, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Februari 23, Simba ikashinda nyumbani kwa mara ya tatu bao 1-0, likiwekwa wavuni na Luis Miquissone, na ndiyo msimu ambao iliongoza kundi, Al Ahly ikashika nafasi ya pili.

**Simba 2-2 Al Ahly (2023)**

Kwa mara ya kwanza, Simba ililazimishwa sare nyumbani dhidi ya Al Ahly katika michuano ya African Football League, mechi hii ilichezwa Oktoba 20, mwaka jana, katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, timu hizo zikimaliza dakika 90 kwa sare ya mabao 2-2. Mabao ya Simba yakifungwa na Kibu Denis na Sadio Kanoute, huku ya Al Ahly yakiwekwa wavuni na Reda Slim na Mahmoud Karhaba.

**Simba 0-1 Al Ahly (2024)**

Ijumaa iliyopita, rekodi ya Simba ya kutopoteza mechi yoyote dhidi ya Al Ahly ikicheza nyumbani ilivunjwa, ilipochapwa mabao 1-0 katika mchezo ya robo fainali Ligi ya Mabingwa, Uwanja wa Banjamin Mkapa, kwa bao lililowekwa wavuni na Ahmed Nabil Koka dakika ya nne ya mchezo.

**Yanga 3-3 Mamelodi Sundowns (2001)**

Ilikuwa ni raundi ya pili ya hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika kati ya Yanga na Mamelodi Sundowns.

Baada ya kufungwa mabao 3-2, Mei 13 nchini Afrika Kusini, zilirudiana Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza Mei 27, 2001 na timu hizo kufungana mabao 3-3.

Kwa bahati mbaya sana, Yanga ikawa imetolewa kwenye michuano hiyo, Mamelodi ikisonga mbele mpaka hatua ya fainali ilipofungwa na Al Ahly ya Misri, kwa sare ya nyumbani Sauzi na kwenda kufa mabao 3-0 nchini Misri.

**Yanga 0-0 Mamelodi Sundowns (2024)**

Jumamosi iliyopita Yanga ililinda rekodi yake ya kutopoteza mechi nyumbani dhidi ya Mamelodi Sundowns, zilipokutana kwa mara ya pili baada ya miaka 23, na kulazimisha suluhu, katika mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

**JE, WAJUA?**




KWA mara ya kwanza Al Ahly kutoka sare na Simba katika Uwanja wa Mkapa ni mwaka jana kwenye michuano ya African Football League zikifungana mabao 2-2 na kwa mara ya kwanza Simba kupata sare Uwanja wa Cairo Misri dhidi ya miamba hiyo ni katika michuano hiyo mchezo wa marudiano matokeo yakiwa 1-1. Pia kwa mara ya kwanza Al Ahly kushinda katika Uwanja wa Mkapa dhidi ya Simba ni Ijumaa iliyopita kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika ikishinda 1-0, je nini kitatokea Ijumaa wiki hii Uwanja wa Cairo, Misri timu hizo zikirudiana?

Nipashe
# Spotika
NIPASHE JUMATATU APRILI 1, 2024



Straika wa Yanga, Clement Mzize, akiwa ameruka juu kupiga mpira kichwa, akisababisha hatari kwenye lango la Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, akichungwa na beki Mosa Lebusa katika mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, iliyochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na kumalizika kwa sare tasa. **MPIGAPICHA WETU**

# YANGA ILIVYOLINDA REKODI CAF YA SIMBA IKIVUNJWA

**Na Adam Fungamwango**

MECHI za kwanza za robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika zilimalizika kwa wawakilishi wa Tanzania, Simba kuchapwa bao 1-0 Ijumaa iliyopita katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, dhidi ya Al Ahly ya Misri, na Jumamosi Yanga kutoka suluhu dhidi ya Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini.

Majaliwa ya timu za Tanzania yapo kwenye mechi za marudiano zitakazochezwa Ijumaa wiki hii, Simba itakapokuwa nchini Misri na Yanga nchini Afrika Kusini ili kujua kama zote mbili au walau moja inaweza kutinga hatua ya nusu fainali.

Kipigo cha bao 1-0 ilichokipata Simba kimehitimisha rekodi nzuri ya timu hiyo kila inapocheza na Al Ahly hapa nchini.

Kwa mara ya kwanza Al Ahly imepata ushindi dhidi ya Simba nchini tangu timu hizo zilipoanza kukutana mara ya kwanza mwaka 1985.

Al Ahly imefanikiwa kuifunga Simba baada ya kucheza mechi nne bila mafanikio kwenye michuano mbalimbali ya kimafataifa hapa nchini.

Simba imeshinda mara tatu na sare moja, kabla ya kupoteza mechi ya Ijumaa, ikiwa ni mchezo wa tano timu hizo kukutana jijini Dar es Salaam.

Kwa upande wa Yanga imefanikiwa kulinda rekodi yake ya mwaka 2001 ya kutoka sare dhidi ya Mamelodi Sundowns. Hii ni mara ya pili timu hizo kukutana nchini na mara zote Yanga imepambana kuhakikisha haipoteza nyumbani.

Katika makala haya tumekusanya rekodi zote za timu hizo zilipochezwa nchini, Simba dhidi ya Al Ahly na Yanga dhidi ya Mamelodi Sundowns na matokeo yake hadi mechi za wiki hii, twende sasa...

**Simba 2-1 Al Ahly (1985)**

Mara ya kwanza Simba ilianza kucheza na Al Ahly, Agosti 22, 1985 kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza, ikiwa ni michuano ya Kombe la Washindi Barani Afrika, sasa Shirikisho, ikishinda mabao 2-1 yaliyofungwa na Zamoyoni Mogella na Mtemi Ramadhani, huku bao la kufutia machozi la Al Ahly likifungwa na Mohamed Ae Khatib 'Bibo' ambaye kwa sasa ndiye rais wa klabu hiyo.

**Simba 1-0 Al Ahly (2019)**

Ilikuwa ni Februari 12, 2019 mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi iliposhinda bao 1-0, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Baada ya kupigwa mabao 5-0, Februari 2 nchini Misri, Simba ilirejea nyumbani na kulipa kisasi hicho kwa bao lililowekwa wavuni na straika, Meddie Kagere. Simba na Al Ahly zote zilisonga mbele kwenye kundi hili.

**Simba 1-0 Al Ahly (2021)**

Timu hizo zilipangwa tena kwenye makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, 2021, na mechi ya kwanza ilicheza nchini kama kawaida, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Februari 23, Simba ikashinda nyumbani kwa mara ya tatu bao 1-0, likiwekwa wavuni na Luis Miquissone, na ndiyo msimu ambao iliongoza kundi, Al Ahly ikashika nafasi ya pili.

**Simba 2-2 Al Ahly (2023)**

Kwa mara ya kwanza, Simba ililazimishwa sare nyumbani dhidi ya Al Ahly katika michuano ya African Football League, mechi hii ilichezwa Oktoba 20, mwaka jana, katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, timu hizo zikimaliza dakika 90 kwa sare ya mabao 2-2. Mabao ya Simba yakifungwa na Kibu Denis na Sadio Kanoute, huku ya Al Ahly yakiwekwa wavuni na Reda Slim na Mahmoud Karhaba.

**Simba 0-1 Al Ahly (2024)**

Ijumaa iliyopita, rekodi ya Simba ya kutopoteza mechi yoyote dhidi ya Al Ahly ikicheza nyumbani ilivunjwa, ilipochapwa mabao 1-0 katika mchezo ya robo fainali Ligi ya Mabingwa, Uwanja wa Banjamin Mkapa, kwa bao lililowekwa wavuni na Ahmed Nabil Koka dakika ya nne ya mchezo.

**Yanga 3-3 Mamelodi Sundowns (2001)**

Ilikuwa ni raundi ya pili ya hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika kati ya Yanga na Mamelodi Sundowns.

Baada ya kufungwa mabao 3-2, Mei 13 nchini Afrika Kusini, zilirudiana Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza Mei 27, 2001 na timu hizo kufungana mabao 3-3.

Kwa bahati mbaya sana, Yanga ikawa imetolewa kwenye michuano hiyo, Mamelodi ikisonga mbele mpaka hatua ya fainali ilipofungwa na Al Ahly ya Misri, kwa sare ya nyumbani Sauzi na kwenda kufa mabao 3-0 nchini Misri.

**Yanga 0-0 Mamelodi Sundowns (2024)**

Jumamosi iliyopita Yanga ililinda rekodi yake ya kutopoteza mechi nyumbani dhidi ya Mamelodi Sundowns, zilipokutana kwa mara ya pili baada ya miaka 23, na kulazimisha suluhu, katika mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

## JE, WAJUA?



KWA mara ya kwanza Al Ahly kutoka sare na Simba katika Uwanja wa Mkapa ni mwaka jana kwenye michuano ya African Football League zikifungana mabao 2-2 na kwa mara ya kwanza Simba kupata sare Uwanja wa Cairo Misri dhidi ya miamba hiyo ni katika michuano hiyo mchezo wa marudiano matokeo yakiwa 1-1. Pia kwa mara ya kwanza Al Ahly kushinda katika Uwanja wa Mkapa dhidi ya Simba ni Ijumaa iliyopita kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika ikishinda 1-0, je nini kitatokea Ijumaa wiki hii Uwanja wa Cairo, Misri timu hizo zikirudiana?



## HABARI DODOMA

# Waziri awataka wafanyabiashara kutumia fursa kuondolewa ushuru

**Na Enock Charles**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji amewataka wafanyabiashara kutumia fursa ya kuondolewa kwa ushuru kwa asilimia 99 kwa bidhaa zitakazohusika kwenye biashara baina ya Tanzania na Uingereza.

Waziri Kijaji ameyasema hayo wakati wa akifungua semina ya wafanyabiashara wa Tanzania na Uingereza katika Mpango wa Biashara kwa Nchi Zinazoendelea (DCTS) wa nchi ya Uingereza Ijumaa iliyopita.

Aliwataka wafanyabishara wa Tanzania kuzalisha bidhaa zenye ubora zitakazokubalika kirahisi katika masoko ya nje hasa Uingereza na kuongeza kiwango cha nchi kuuza bidhaa nje kuliko kuingiza jambo ambalo linaikosesha nchi mapato ya fedha za kigeni.

Alisema kwa mwaka 2023 Tanzania iliuza Uingereza bidhaa zenye thamani ya Sh.Bilioni 46, lakini ilinunua bidhaa zenye thamani ya Sh.trilioni 4 akiwataka wafanyabishara kuongeza kiwango cha kuuza zaidi kuliko kutegemea kununua bidhaa kutoka nje ikiwemo Uingereza.

"Semina hii ya Wafanyabiashara wa Uingereza na Tanzania itasaidia wafanyabiashara wetu kuelewa ni bidhaa gani na ni viwango gani vinavyohitajika vya bidhaa zinazosafirishwa nje ya nchi, taratibu za mauzo ya nje ili Watanzania waweze kufaidika na soko la Uingereza," alisema Waziri Kijaji.

Mpango huo wa Serikali ya Uingereza una lengo la kuunda ushirikiano mpya baina ya Wafanyabiashara katika mataifa yaliyo chini ya mpango huo na mamlaka ya biashara ya nchi hiyo kwa faida ya pande zote mbili.

Dk.Cecilia Houser mtaalamu wa Intelijensia ya Biashara na Masoko kutoka Kituo cha Biashara cha Kimataifa alisema Tanzania inaweza kuongeza nguvu ya uzalishaji katika bidhaa ambazo ina uwezo nazo kama vile chai, parachichi na kahawa kupeleka katika masoko ya Uingereza na kuongeza kipato kwa wafanyabishara wake.

Alisema miongoni mwa biashara kubwa zinazofanyika baina ya mataifa yanayoendelea chini ya mpango huo ni mboga, matunda na pamba na kwamba kiasi cha paundi 173,000 kiliokolewa kutokana na mpango huo.

Aidha, alishauri nchi zilizo chini ya mpango huo kuitumia vizuri fursa hiyo.

Mfanyabiashara Hezron Charles aliyehudhuria semina hiyo alisema semina hiyo itawezesha wafanyabishara kujua viwango vinavyohitajika katika biashara baina ya Uingereza na Tanzania na pia sheria na taratibu za kibiashara za kimataifa jambo litakalosaidia kupunguza vikwazo vya kibiashara na kuongeza uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi.




Mkuu wa Gereza la Isanga, ACP, Zefania Neligwa (kushoto) akipokea misaada ya vyakula kutoka kwa Katibu wa Bakwata wilaya ya Dodoma Ahmed Msuri (kulia ) kwa niaba ya viongozi wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania wilaya ya Dodoma vilivyotolewa kwa ajili ya kuwasaidia mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani baada ya kuwatembelea jana

## Mkuu wa Gereza awaita wasamaria kuwasaidia wafungwa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Gereza la Isanga mkoani Dodoma, Neligwa Zefania amewaomba wadau kuwakumbuka wafungwa na mahabusu kwa kuwapatia misaada itakayosaidia kuipunguzia serikali mzigo wa kuwahudumia.

Alitoa wito huo mwishoni mwa wiki alipokuwa akipokea misaada ya vyakula mbalimbali iliyotolewa na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Wilaya ya Dodoma kwa ajili ya kuwasaidia wafungwa na mahabusu.

Mkuu huyo alisema kuwa mara nyingi wafungwa waliopo magerezani wamekuwa wakisahaulika katika kusaidiwa misaada mbalimbali tofauti na jamii zingine kama vile wajane na yatima ambao wamekuwa wakikumbukwa kila wakati.

"Humu gerezani licha ya misaada mingine inayotolewa na wafadhili mbalimbali pia tunahitaji kusaidia hata na vifaa vya michezo kama vile bao la kuchezea, Draft, mipira hii itasaidia na wao kutengeneza afya ya akili na kuonesha vipaji vyao," alisema.

Mwenyekiti wa BAKWATA Wilaya ya Dodoma, Bashiru Omary alisema kuwa Watanzania wakijijengea tabia ya utamaduni wa kuwakumbuka wafungwa na mahabusu magerezani watakuwa wameipunguzia mzigo serikali kwa huduma wanazo wahudumia.

"Tunaomba taasisi za kidini, mashirika mbalimbali na watu binafsi kuisaidia serikali katika kuwapatia misaada ambayo inayoweza kuwapunguzia changamoto wanazokutana nazo wafungwa na mahabusu," alisema.

Alisema BAKWATA wilaya imekuwa na tamaduni ya kuwakumbuka jamii yenye uhitaji kila wakati kulingana na mahitaji yanayohitajika hasa wakati wa mwezi wa Ramadhani.

Katibu wa Jumuiya ya Wanawake wa Kiislamu Tanzania (JUWAKITA) Wilaya ya Dodoma, Zainabu Mtoro, aliziomba taasisi za wanawake kuungana na serikali ambayo imekuwa na mzigo mkubwa wa kuwatunza wafungwa na mahabusu magerezani.

# 'Waganga wakuu anzisheni utalii wa matibabu'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAGANGA wakuu wa mikoa na wilaya wametakiwa kuweka mipango ya kuwa na utalii wa kimatibabu kwenye maeneo yao, kuwa na huduma bora za afya zinazovutia ngazi ya afya ya msingi.

Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Rufaa nje ya nchi kutoka Wizara ya Afya, Dk. Asha Mahita alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa akitoa mada kuhusu utalii wa kimatibabu ngazi ya afya ya msingi katika mkutano wa afya wa kimataifa uliofanyika jijini Dodoma.

Alisema serikali imefanya uwekezaji mkubwa wa miundombinu na vifaa tiba, hivyo wahakikishe kwenye maeneo yao wanatumia fursa hiyo.

"Tuchukue kuanzia sasa mgonjwa anayekuja bila rufaa kwenye hospitali ni utalii wa kimatibabu, tukijipanga vizuri suala hili ni sehemu inayoongeza mapato katika hospitali. Na hii ni kwamba mtu anaweza kutembea kutoka eneo moja kwenda lingine kwa kuvutiwa na huduma, utalii wa matibabu ni biashara," alisema.

Alisema inakadiriwa kuwa ifikapo mwaka 2032 katika soko la utalii wa matibabu duniani kiasi cha Dola za Marekani bilioni 346.1 zitaingizwa, hivyo ni muda wa Tanzania kutilia mkazo eneo hilo.

"Kwa mfano kwa mwaka 2022/23 tulipokea wagonjwa waliohitaji matibabu nchini 6,472 na mwaka 2023 hadi Februari 2024 tumepokea 6,963 kwa hiyo waganga wakuu wa mikoa na wilaya mtakaporudi angalieni huduma mnazotoa, mna ubingwa gani ili eneo la utalii wa matibabu liimarishe uchumi sekta ya afya," alisema.

Dk.Liggy Vumilia kutoka Wizara ya Afya alisema katika kukabiliana na upungufu wa watoa huduma za afya uliopo hospitali za ngazi ya afya ya msingi zinapaswa kuwa na mfumo wa tiba mtandao, ili watu wengi wafikiwe na kupata huduma bobezi badala ya kusafiri umbali mrefu kufuata huduma.

Alisema wamelenga kupeleka hizo huduma nchi nzima ili kila mtu apate huduma bora na daktari katika ngazi ya afya ya msingi awe na ana uwezo wa kuwasiliana na daktari bingwa aliyepo Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Saratani ya Ocean Road na Hospitali ya Benjamin Mkapa.



# Wanne mbaroni tuhuma wizi mota za mashine za kusaga

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JESHI la Polisi Mkoa wa Njombe linawashikilia watu wanne kwa tuhuma za kujihusisha na matukio ya wizi wa mota za mashine ya kusaga nafaka, zilizoibiwa kwenye maeneo tofauti mkoani hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi Mahamoud Banga aliwataja watuhumiwa ni Betod Mtitu (38) Emmanuel Chengula (24), Nassoro Chura (35) na Omary Manga (42).

Alisema baada ya kukamatwa kwa mtuhumiwa Betod Mtitu jeshi hilo lilifanikiwa kukamata mota 20 katika maeneo mbalimbali ikiwemo mkoani Iringa, wilayani Wanging'ombe na Njombe.

Kamanda Banga alisema baada ya wizi huo watuhumiwa hao walikwenda kuziuza na zingine kuzificha.

Wakati huo huo, Kamanda Banga alisema pia jeshi hilo linawashikilia watu wengine wawili Nerbert Mehenge (54) na Tesifora Mgaya (32) wakiwa na gari aina ya Toyota Carina yenye namba za usajili T 461CKA ambalo wanadaiwa kulitumia katika kutapeli watu wakijifanya wanauza madini.

"Hawa watu wanajihusisha na masuala ya utapeli wa madini ya dhahabu na hapa Njombe wamekuwa wakifanya utapeli wa madini ya dhahabu na wamepora watu mbalimbali," alisema Banga.

Alisema baada ya kukamatwa na kupekuliwa walikutwa na simu sita, madini feki, tochi tatu za kumulikia madini na vibao vya kuwadanganyia watu kuwa ni fedha pamoja na bahasha tupu 10.

Alisema watuhumiwa hao wamefikishwa mahakamani kwa baadhi ya makosa ya utapeli lakini uchunguzi unaendelea.

Alisema sambamba na hilo Jeshi la Polisi linawashikilia watuhumiwa watatu wilayani Ludewa kwa kosa la mauaji ya Rainel Mapunda (60) mkazi wa Kimelembe.

Kamanda Banga alisema Rainel aliviziwa akiwa anatoka kwenye kilabu cha pombe ya kienyeji na kujeruhiwa kwenye paji la uso na shingoni na kitu chenye ncha kali.

Alisema chanzo cha mauaji hayo ni imani za kishirikina ambapo marehemu anatuhumiwa na kifo cha mwanae wa kiume aliyefariki kwa ajali ya gari mkoani Ruvuma.

Kamanda Banga alisema: "Chanzo hawa ndugu walikuwa wanamtuhumu kuwa ajali ile imesababishwa na huyu marehemu ambaye ameuawa".



Mkuu wa Wilaya ya Ludewa Mkoa wa Njombe, Victoria Mwanziva (wapili kushoto) pamoja na waumini wa dini ya kiislamu wilayani humo wakiwa katika dua/kisomo maalumu cha kumuombea Rais Dk. Samia Suluhu Hassan iliyofanyika katika msikiti wa wilaya hiyo mwishoni mwa wiki. **PICHA: ELIZABETH JOHN**

# Wafanya dua kumwombea Samia apate hekima, baraka

**Na Elizabeth john,** LUDEWA

VIONGOZI wa serikali pamoja na wananchi wilayani Ludewa mkoani Njombe wamefanya dua/kisomo maalum cha kumuombea Rais Samia Suluhu Hassan ili azidi kupata kheri, hekima na baraka.

Akizungumza mwishoni mwa wiki baada ya kufanyika kwa kisomo hicho katika Msikiti wa Wilaya ya Ludewa, Mkuu wa wilaya hiyo, Victoria Mwanziva alisema Rais Samia analiongoza vyema taifa hivyo anapopata baraka na taifa zima linapata baraka pia kupitia yeye.

"Rais wetu amekuwa ni kiongozi bora na mwenye hekima, hivyo hatuna budi kumwombea kwa Mungu ili aweze kuendeleza ubora alionao na kile ambacho Mungu amekiweka ndani yake," alisema Mwanziva.

Mwanziva alisema lengo la kuomba dua hiyo ni kwa ajili ya kuendelea kuyaenzi mengi mazuri anayoyafanya ndani ya wilaya hiyo na Tanzania, haswa kwenye miradi mbalimbali ya kimaendeleo.

"Miradi mingi imeletwa wilayani Ludewa, hivyo sisi kama viongozi na Watanzania kwa ujumla tunayo sababu ya kumuombea Rais wetu ili aweze kufanya mambo makubwa zaidi kwa ajili ya maendeleo yetu," alisema Mwanziva. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, Sunday Deogratius alisema Rais Samia amefanya maendeleo makubwa katika halmashauri hiyo.

Shekhe wa Wilaya ya Ludewa, Haruna Rahim alimshukuru Mkuu wa Wilaya kwa kuwaunganisha katika kufanya kisomo hicho pamoja na kupata futari. Alisema kwa kufanya hivyo kunaongeza swawabu kutoka kwa Mungu na hasa katika kipindi hiki cha mfungo wa Ramadhan.

Kisomo hicho kiliambatana na futari iliyoandaliwa na Mkuu wa Wilaya Victoria Mwanziva.

# Makete yapokea bil. 20/- utekelezaji miradi miaka 3 ya Samia

**Na Elizabeth John,** MAKETE

HALMASHAURI ya Wilaya ya Makete mkoani Njombe kwa kipindi cha miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan imepokea Sh. bilioni 20 zilizotumika katika miradi mbalimbali ikiwemo ya afya na elimu.

Mkurugenzi wa Hamashauri ya Wilaya ya Makete, Willium Makufwe aliyasema hayo wakati akieleza mafanikio ya Rais Samia katika miaka mitatu ya uongozi wake.

Alisema hivi sasa wanaendelea na ujenzi wa ofisi za kisasa za halmashauri na wamepokea shilingi bilioni mbili.

"Huu mradi tuafanya chini ya mkandarasi mjenzi MUST na mnaona hata tulivyoingia vifaa vya ujenzi vipo kwa hiyo ninachowaomba wenzetu wa MUST waongeze kasi ya ujenzi. Ni kweli Makete tunachangamoto ya mvua zinanyesha lakini watumie nafasi vizuri na wafanye kazi kwa tija ili jengo liweze kukamilika na kutoa huduma inayostahili," alisema Makufwe.

Makufwe alisema miradi mingine ipo katika Shule ya Sekondari Iwawa, madarasa 12, Sekondari Usililo madarasa 12, Sekondari Mount Chafukwe madarasa 12.

"Katika kipindi cha miaka hii mitatu Rais Samia ameleta hapa zaidi ya Sh. bilioni 20 na kwa uchache tu tuna vituo vya afya karibia vitano kwa hiyo ninachowaomba wanamakete hasa wazazi na walezi lazima tuiunge mkono serikali" aliongeza Makufwe.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Makete, Dk. Jonathan Kitundu alisema katika kipindi cha miaka mitatu wamepata fedha kwa ajili ya ukarabati wa hospitali pamoja na ujenzi wa jengo la huduma za dharura.

Kwa upande wa sekta ya elimu miongoni mwa shule iliyopata maboresho makubwa ni pamoja na Shule ya Sekondari Lupalilo ambapo Makamu Mkuu wa Shule hiyo, Kilatu alisema shule hiyo ilikuwa na changamoto kubwa kwenye miundombinu na kuwalazimu wazazi kuchangia mara kwa mara kwa ajili ya ujenzi.

Miongoni mwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Lupalilo wakiwemo Respoka Mahenge na Leokadia Nyika walimshukuru Rais Samia kwa ujenzi wa miundombinu hiyo na kuahidi kwenda kufanya vizuri kwenye mitihani yao.

Mmoja wa wakazi wilayani Makete, Daima Kilale alisema halmashauri hiyo imekuwa na maendeleo makubwa hususani kwenye maboresho ya miundombinu, huku wakibainisha kuwa awali katika maeneo mengi hususani kwenye Hospitali ya Wilaya ambapo vitanda vilikuwa vichache lakini pia visivyokuwa na ubora ukilinganisha na sasa.



## Serikali yajinasibu kuboresha mazingira bora ya kujifunzia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Abdulgulam Hussein amesema serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri ya kujifunzia ili watoto waweze kupata elimu bora.

Aliyasema hayo juzi visiwani Zanzibar wakati wa hafla ya utiaji saini mkataba wa uchapishaji vitabu kwa ajili ya shule binafsi Zanzibar, kati ya Wizara na kampuni ya SEMUKA International Ltd ya jijini Dar es salaam.

Alisema lengo kuu la serikali ni kuona wananchi wake wanapata elimu bora, ndiyo maana kumekuwa na jitihada mbali mbali za kuhakikisha dhamira na malengo yake wanafikiwa.

Alisema kuwa lengo serikali ni kuimarisha miundombinu na huduma katika shule za Zanzibar, linalenga kuimarisha ubora wa elimu inayotolewa kwa wanafunzi wa shule za serikali na binafsi.

"Leo hapa tumeshuhudia utiaji wa saini wa mkataba huu wa uzalishaji wa vitabu ambapo muda siyo mrefu taasisi ya elimu imeanza kugawa vitabu katika shule za serikali na itafanya vile vile kwa uchache wake kwa shule binafsi," alisema.

Aidha alisema vitabu hivyo haviuzwi na walimu watatumia kwa kusomeshea, ila kama itatokea mzazi anataka vitabu hivyo anapaswa kununua kulingana na utaratibu utakaowekwa.

Hivyo alisema ni jukumu la taasisi inayosimamia shule binafsi kuitangaza na muda si mrefu wanaamini wazalishaji hao wataingiza sokoni na lengo la serikali kuwafikia watu wao.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, khamis Abdulla said, alisema utiaji saini wa mkataba huo ni kuandika historia katika katika sekta ya elimu ambapo kwa mara ya kwanza kutachapwa vitabu ambavyo watakuwa wanavigawa kwa shule binafsi.

Alisema lengokubwa ni kuhakikisha kwamba ubora wa elimu katika nchi yao unafanana.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Elimu Zanzibar, Abdalla Mohamed Mussa, alisema kuwa hatua hii imefikiwa ili kuona kwamba hakuna utofauti baina ya shule za serikali na binafsi katika mitaala yao.

Naibu Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Shule binafsi Zanzibar (ZAPS), Mbarouk Shaaban Haji, aliishukuru wizara kwa kuwapa ushirikiano mkubwa katika kuendeleza elimu Zanzibar.

Meneja Masoko wa SEMUKA, Walii Hassan Miyonga alisema mchakato wa kuandaa watoto ni mkubwa katika kuhakikisha wanapata elimu bora.

Alisema wanaahidi kuwa mchakato wa uletaji wa vitabu hivyo hautachukuwa muda na ndani ya miezi miwili watakuwa tayari wameshaleta.

# Kamati yaagiza utambuzi maeneo kuepuka migogoro ardhi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMATI ya Ardhi ya Baraza la Wawakilishi imeitaka Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kuzipatia ufumbuzi changamoto zote zinazohusiana na masuala ya ardhi, ikiwemo kufanya utambuzi wa maeneo mapya.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Yahya Abdalla Rashid alitoa maagizo hayo juzi alipokuwa akizungumza na watendaji wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi visiwani Zanzibar, wakati kamati ikipokea Ripoti ya Mthamini Mkuu wa Serikali na Kamisheni ya Ardhi.

Alisema ripoti hiyo imebainisha changamoto nyingi ikiwemo masuala ya utendaji na upungufu wa vitendea kazi kwa watumishi.

Alisema wakati umefika wizara kupitia Kamisheni ya Ardhi kuzipatia ufumbuzi changamoto za migogoro ya ardhi ikiwemo katika maeneo ya ukanda wa fukwe za bahari.

Alisema migogoro mingi imeibuka katika maeneo hayo ambapo wananchi na wawekezaji wameingia katika mivutano kufuatia maeneo hayo kuongezeka thamani ya ardhi kwa shughuli za miradi ya uwekezaji.

"Wakati umefika kwa wizara kuipatia ufumbuzi migogoro ya ardhi ambayo imewakumba wananchi pamoja na wawekezaji katika maeneo ya fukwe za baharini"alisema.

Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, Salha Mohamed Mwinjuma, alisema wamejipanga kushughulikia changamoto za migogoro ya ardhi kwa wawekezaji.

Alisema serikali ipo katika hatua za mwisho za kuunda chombo kitakachoshughulikia migogoro ya ardhi na kuipatia ufumbuzi haraka.

"Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji tupo katika hatua za mwisho za kutayarisha chombo kitakachoshughulikia migogoro ya ardhi zaidi katika miradi ya wawekezaji"alisema.

Baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano Ardhi na Nishati waliitaka Kamisheni ya Ardhi kuitambua ardhi yote nchini kwa kuirasimisha hatua ambayo kwa kiasi kikubwa itapunguza migogoro ya ardhi.

Walisema changamoto nyingi za ardhi zimechangiwa na Kamisheni ya Ardhi kushindwa kuihakiki ardhi yote kwa ajili ya kupanga matumizi sahihi.



Askofu Augustino Shao akimbatiza Piero Modestus kwenye Ibada ya mkesha wa Pasaka katika Kanisa la Mtakatifu Joseph mjini Zanzibar jana. Kushoto ni msimamizi wake Julius Mnyagala. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Wanafunzi 2,000 wapatiwa elimu kujikinga mimba za utotoni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANAFUNZI zaidi ya 2,000 wa shule za sekondari wanatarajiwa kupatiwa elimu ya afya ya uzazi, ili kujiepusha na mimba za utotoni pamoja na kujitambua.

Akifunga mafunzo ya afya ya uzazi jana kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mtule Mkoa wa Kusini Unguja, Ofisa Msaidizi wa mradi huo, Judith Maduhu alisema kwa awamu ya kwanza wameshatoa elimu hiyo kwa wanafunzi 700 Kisiwani Pemba ikiwemo Shule ya Shumba Viamboni na Chwaka tumbe.

Alisema lengo ni kuhakikisha wanafunzi wanafahamu athari za mimba za umri mdogo na kuepukana nazo

mafunzo ahayo yalitolewa na mradi wa Food for the Hungary International (KFHI) chini ya ufadhili wa Shirika la Koica.

Alisema malengo ya mradi huo ni wanafunzi kuwa salama na mazingira hatarishi ya uzazi wa mapema wakati wakiwa shuleni na katika mazingira mengine wakati bado wanahitaji kupata elimu kwa mustakbali mzuri wa maisha yao ya baadae.

"Kwa shule hii ya Mtule tumetoa mafunzo ya afya ya uzazi kwa wananfunzi 326 na tutaendelea kwa shule zingine zilizomo katika mradi ikiwemo Shule ya Jendele na Fukuchani kwa upande wa Unguja" alisema Maduhu.

Aidha alisema mradi huo hauwalengi wanafunzi pekee katika kuwapa mafunzo hayo bali hata walimu wa shule hizo, ili kuwa rahisi kuwakumbusha wanafunzi pale wanapohitaji msaada na ushari nahisi kuhusu makuzi yao.

"Vijana wengi wakiathirika katika utumiaji wa dawa za kulevya kutokana na makundi wanayofutana nayo wakiwa mitaani jambo ambalo limekuwa likiathiri ndoto zao za baadaye"alisema Maduhu.

Mwalimu msimamizi wa mafunzo katika Shule ya Mtule, Sayyidat Ali Hamad, alisema mafunzo hayo yamekuja wakati sahihi kwa sababu wanafunzi wengi wanapofika katika umri wa balehe wanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo mihemko na kusababisha kupata mimba za umri mdogo.

Alisema hivi sasa dunia inakwenda na wakati, hivyo wanafunzi wengi hutumia mitandao kupitia simu kwa kuangalia picha zisizo na maadili.

Wanafunzi waliopatiwa mafunzo hayo, walisema yatawafanya kujitambua katika harakati zao za kutafuta elimu na kujiepusha na viashiria vinavyosabisha kujiingiza katika vitendo viovu.

MAKALA MAALUM

# TAMFI waangazia nafasi ya wanawake ustahimilivu wa mazingira, uwezeshaji kifedha



Washiriki wa mkutano katika picha ya pamoja

**Na Mwandishi Wetu**

IKIANGAZIA muunganiko wa kipekee wa uwezeshaji jinsia, utetezi wa mazingira, na fedha, Shirikisho la Asasi za Kifedha Tanzania (TAMFI), limeongoza mkutano wa "Wanawake katika fedha: Kukumbatia mabadiliko ya tabianchi" mjini Dar es Salaam, Machi 26, mwaka huu.

Mkurugenzi Mtendaji wa TAMFI, Winnie Terry, ameonyesha umuhimu wa mkutano huo kama jitihada ya kuchanganya jinsia na uendelevu wa mazingira ndani ya sekta ya fedha.

"Ahadi yetu ya 'Kukumbatia Mabadiliko ya Tabianchi' inazidi mjadala tu; ni wito wa kuchukua hatua. Kwa kulingana na jitihada za kiuongozi za serikali ya awamu ya sita chini ya Uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, tunalenga kuchangia kwa maana kubwa katika uhifadhi wa mazingira na kupambana na ukataji miti kupitia mipango ya kupika kwa usafi. Hii inaendana kikamilifu na mpango wetu mkakati, ikisisitiza umuhimu wa kujihusisha kwa vitendo katika uendelevu."

Terry alielezea umakini wa shirikisho hilo katika kushughulikia vipengele muhimu vya maji, nishati mbadala, na mabadiliko ya tabianchi na kujitolea kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu 14 na njia ya kimkakati iliyochukuliwa kwa kuhusisha paneli mbili tofauti. Paneli moja ilijumuisha viongozi kutoka mashirika mbalimbali, wakati nyingine iliingiza mtazamo kutoka kwa wanufaika na wakopaji.

Alisema kwamba, kukumbatia mabadiliko ya tabianchi, katika muktadha huu, inamaanisha kuelewa na kupambana na mabadiliko ya tabianchi kama wafadhili. Terry alisisitiza kusudi la tukio hilo kuonyesha jukumu muhimu la wanawake katika fedha, juhudi hii ya kimataifa, ikiwaonyesha umuhimu wa mchango wao katika uendelevu wa mazingira.

Mkutano huo, uliopata ufadhili kutoka kwa Foundation ya Charles Stewart Mott, uliweka wazi ushawishi muhimu wa taasisi za kifedha katika kuunga mkono mazoea endelevu, kwa kuzingatia hasa kuwezesha wanawake ndani ya sekta ya fedha kuongoza jitihada hii muhimu. Ilirahisisha mijadala kuhusu mwingiliano kati ya operesheni za kifedha na mabadiliko ya tabianchi, iliwahamasisha washiriki kuchukua hatua rafiki kwa mazingira ndani ya taasisi zao na kuendeleza jumuiya ya wanawake katika fedha ambao ni watetezi wa utunzaji wa mazingira.

Terry alisisitiza mabadiliko makubwa kuelekea mazoea endelevu ya maisha, yakionyesha ahadi ya Tanzania kupunguza athari za mazingira na kuboresha matokeo ya afya kwa wanawake. Wanawake katika fedha wanapaswa kuwa mabingwa wa msukumo huo.

Msemaji mkuu katika mkutano huo, Devotha Ntuke Minzi, Mwenyekiti wa Bodi ya TAMFI, alisisitiza jukumu muhimu la wanawake katika kushughulikia mabadiliko ya tabianchi na kusonga mbele usawa wa jinsia. "Tunapoadhimisha Mwezi wa Kimataifa wa Wanawake, hebu tutambue athari kubwa wanawake katika fedha wanaweza kuwa nayo katika kukuza uendelevu wa mazingira na usawa wa jinsia," Minzi alisema.



Mkurugenzi Mtendaji wa TAMFI, Winnie Terry, akiongea kwenye mkutano.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Akisisitiza athari zisizo sawa za mabadiliko ya tabianchi kwa wanawake, hasa Tanzania na kote duniani, Minzi aliita kwa njia shirikishi ya kufanya maamuzi na mipango ya vitendo. Alihimiza haraka ya kuongeza sauti za wanawake katika fedha kama waendeshaji muhimu wa suluhisho endelevu kwa changamoto hizi za kimataifa. Alisisitiza umuhimu wa ushirikiano na mshikamano katika sekta, taaluma, na vizazi ili kupata maendeleo yenye maana.

"Usawa wa jinsia na uendelevu wa mazingira vinaunganishwa kwa asili," Minzi alibainisha, akionyesha jukumu kuu wanawake wanalocheza katika uhimili wa hali ya hewa na mipango ya maendeleo endelevu. Aliwatetea wanawake katika fedha kama mkakati wa kufungua suluhisho bunifu na shirikishi kwa faida ya jamii kwa ujumla.

Deodati Bernard, Afisa Programu TAMFI, alisisitiza mchango mkubwa wa wanawake kwa maendeleo ya Tanzania na uongozi wa kimataifa katika fedha na ujasiriamali.

"Tanzania ni nyumbani kwa wanawake zaidi ya milioni 31 na mara nyingi husemwa, 'Ikiwa unataka sababu yako ifanikiwe, mkabidhi mwanamke,'" Bernard alitambua athari kubwa na uaminifu wa wanawake katika kuongoza mipango na kusonga mbele maendeleo.

Mkutano huo ulijivunia ushiriki kutoka kwa wawakilishi wa wanawake na Wakurugenzi Mtendaji kutoka Taasisi za Fedha za Daraja la Kwanza na la Pili, pamoja na wajumbe kutoka Chama cha Benki Tanzania (TBA), Chama cha Nishati Mbadala Tanzania (TAREA), Mtandao wa Maji na Usafi Tanzania (TaWaSanet), New Faces New Voices (NFNV), Amshaamsha Foundation, IMED Foundation, Elico Foundation, Water.org, Kampuni ya Huduma za Nishati Endelevu (SESCOM) na wanawake katika nyanja mbalimbali za mfumo wa mabadiliko ya tabianchi nchini.

TAMFI ni shirika lisilo la kiserikali lenye umuhimu mkubwa linalounganisha taasisi za kifedha ndogo ndogo nchini Tanzania. Lilianzishwa mwaka wa 2001, likihudumu kama mtandao mkuu wa nchi kwa shughuli za kifedha ndogo ndogo, likijivunia uanachama anuwai unaohusisha benki za kibiashara na jamii, NGOs, MFI binafsi, SACCOS, na watoa huduma mbalimbali za biashara. Dhamira ya TAMFI inajikita katika kuimarisha uwezo wa sekta ya kifedha ndogo ndogo kupitia utetezi, ujenzi wa uwezo, utafiti, na kukuza mazoea ya kifedha ndogo ndogo yenye majukumu.

Ikiwa imeongozwa na katiba imara na inaendeshwa na wanachama wake kupitia mikutano ya mwaka ya wanachama, mwelekeo mkakati wa TAMFI uko wazi: kukuza mtandao wa kifedha ndogo ndogo ulio hai ambao unaunga mkono kwa ufanisi sekta ya kifedha ndogo ndogo ya Tanzania. Hii inafanikiwa kwa kutetea mifumo inayofaa ya kisheria, kufanya utafiti husika, na kuhakikisha wanachama wake wanafuata mazoea bora katika kifedha ndogo ndogo, yote haya wakati wa kukuza uwajibikaji, uwazi, na uendelevu.

## HABARI KIMATAIFA

# Papa Francis ahimiza amani ujumbe wa Pasaka

**VATICAN,** Roma

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki duniani Papa Francis ameuhimiza ulimwengu upinge mantiki ya kutumia silaha na kulaani vita vinavyoendelea katika baadhi ya maeneo ikiwemo Ukraine, Gaza, Sudan na Myanmar akisema migogoro hiyo ni upuuzi.

Papa Francis aliyasema hayo jana katika ujumbe wake wa Pasaka katika makao makuu ya kanisa Katoliki Vatican, akirudia wito wake wa kusisitiza kusitishwa kwa mapigani huko Gaza, akitaka misaada zaidi ipelekwe katika eneo hilo na kutaka mateka wanaoshikiliwa na kundi la Hamas waachiwe huru

Papa Francis alipendekeza mabadilishano ya wafungwa wote kati ya Russia na Ukraine, huku akiwasisitiza viongozi wa dunia kufanya juhudi kupambana na biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu na kuwaokoa wahanga.

"Tusiruhusu upepo wa vita uvume Ulaya na eneo la Mediterania, tusikubali mantiki ya matumizi ya silaha na kujihami tena na silaha," alisema

Ilielezwa kuwa takribani waamini 30,000 walihudhuria misa hiyo, na kwamba kelele za shangwe zilisikika wakati kiongozi huyo alipopitishwa kando ya umati wa watu baada ya misa, wengi wakisema Papa aishi muda mrefu.

Maadhimisho ya Pasaka ya Vatican yamegubikwa na wasiwasi kuhusu kiongozi huyo wa kanisa Katoliki duniani ambaye hali yake ya afya imekuwa mbaya kwa miezi kadhaa.

Usalama uliimarishwa kama ilivyo ada kila mara, lakini umeimarishwa zaidi mwaka huu kutokana na shambulizi la kigaidi kwenye ukumbi wa tamasha karibu na mji wa Moscow nchini Russia, huku kundi la kigaidi la Islamic State, likidai kuhusika.

Ilielezwa kuwa kumekuwa na foleni ndefu kwenye malango ya kuingilia uwanja wa Mtakatifu Petro wakati polisi wa Italia walipofanya upekuzi. Na kwamba misa hiyo ni tukio kubwa la Pasaka na ndilo tamasha muhimu katika kalenda ya Kikristo.



Katika Jumapili ya Pasaka, wakristo husherehekea ufufuo wa Yesu Kristo na hivyo ushindi wa uzima dhidi ya kifo. **DW**

# Saa zamuweka matatani Rais Peru

**LIMA,** Peru

MAOFISA wa Polisi nchini Peru wamevamia nyumba ya Rais wa nchi hiyo, Dina Boluarte kama sehemu ya uchunguzi unaoendelea wa ufisadi unaohusiana na saa za kifahari za Rolex zinazomilikiwa na kiongozi huyo, hatua iliyolaaniwa vikali na serikali.

Kwa mujibu wa waraka wa polisi ambao ulinukuliwa na shirika la habari la AFP, takriban maofisa 40 walihusika katika uvamizi huo juzi asubuhi, ambao ulikuwa unatafuta saa za kifahari aina ya Rolex ambazo Rais Dina hakuwa amezitangaza hadharani.

Ilielezwa kuwa Rais huyo anaekabiliwa na misukosuko hakuonekana kuwa nyumbani wakati huo, huku Waziri Mkuu Gustavo Adrianzen akilaani uvamizi huo akisema ni ghadhabu isiyovumilika na iliyovuka mipaka na ni kinyume cha katiba.

**Kashfa hiyo iliibuka baada ya chombo cha habari cha 'La Encerrona' kuripoti katikati mwa mwezi Machi kwamba Rais Dina alikuwa amevaa saa mbalimbali za Rolex kwenye hafla rasmi.**

Maofisa walianzisha uchunguzi dhidi ya Rais Dina mwezi huu baada ya chombo cha habari kusambaza picha za saa zake za kifahari za michezo kwenye hafla za umma.

Pia ilibainishwa kuwa maofisa wa serikali walionekana wakiizunguka nyumba hiyo katika Wilaya ya Surquillo mjini Lima huku wakizuia magari yaliyotaka kuingia eneo hilo, na kwamba tukio hilo la kushtukiza, liliombwa na mwendesha mashtaka wa umma na kuidhinishwa na Mahakama Kuu ya Upelelezi wa Awali.

Ilielezwa kuwa Rais Dina aliingia katika mzozo wa kisiasa kwa kuanzishwa uchunguzi ili kubaini iwapo amejitajirisha kinyume cha sheria akiwa madarakani.

Aidha, ilielezwa kuwa iwapo kiongozi huyo atakutwa na kesi ya kujibu, mashtaka dhidi yake hayataweza kuendeshwa hadi baada ya muhula wake kukamilika Julai 2026 au aondolewe madarakani, kwa mujibu wa katiba.

Baadae mamlaka ya udhibiti serikali ilitangaza kuwa ingepitia matamko ya mali ya kiongozi huyo kutoka miaka miwili iliyopita ili kutafuta kasoro zozote. Huku Rais huyo akijitetea kwamba aliingia ikulu akiwa na mikono misafi na atatoka akiwa na mikono misafi.

Akijibu maswali kuhusu jinsi alivyoweza kumudu saa za bei ghali kwa mshahara wa umma, alisema saa hizo ni zao la kufanya kazi kwa bidii tangu alipokuwa na umri wa miaka 18.

Kashfa hiyo iliibuka baada ya chombo cha habari cha 'La Encerrona' kuripoti katikati mwa mwezi Machi kwamba Rais Dina alikuwa amevaa saa mbalimbali za Rolex kwenye hafla rasmi. Chombo hicho kiliangazia saa hizo kwa kuchapisha picha za kuanzia Desemba 2022, wakati alipochukua madaraka.

Wakili huyo na makamu wa rais wa zamani aligeuka rais wa kwanza mwanamke wa Peru baada ya kiongozi wa mrengo wa kushoto Pedro Castillo kujaribu kulivunja Bunge na kutawala kwa amri, na kusababisha kuondolewa madarakani na kukamatwa. **DW**



Waamini wa dini ya Kikristo huko mjini Vatican wakiwa katika uwanja wa Mtakatifu Petro, wakati wa misa ya Pasaka, jana. **PICHA MTANDAO.**

# Kiongozi wa genge Haiti aionya Kenya

**PORT-AU-PRINCE,** Haiti

KIONGOZI wa genge nchini Haiti, Jimmy Chérizier, ametoa onyo kwa maofisa wa Polisi wa Kenya wanaosubiri kutumwa nchini humo kwa misheni ya kulinda amani, akidai kwamba watakutana na upinzani wa silaha.

Kenya imeahidi kutuma maofisa 1,000 wa polisi kuongoza muungano unaoungwa mkono na Umoja wa Mataifa (UN) ili kusaidia kurejesha hali ya utulivu katika taifa hilo ambalo siku chache zilizopita lilivamiwa na magenge yenye silaha.

Barbeque, alieleza juzi kwamba kikosi chochote cha kigeni cha kulinda amani kinachotumwa katika taifa la Karibea kitakabiliwa na upinzani wa silaha.

"Inabadilika, iwapo wanajeshi wa Kenya au polisi watakuja, vyovyote vile, nitawachukulia kama wavamizi, tutawachukulia kama wavamizi, na hatutakiwi kushirikiana na wavamizi wowote ambao wamekuja kutembea juu ya uhuru wetu," alisema.

Kwa mujibu wa Barbeque, endapo polisi wa Kenya na misheni nyingine za kimataifa zitaingia nchini humo zitafanya mauaji katika jamii masikini. Huku akidai kuwa mawazo ya awali yalifahamisha misheni kuhusu kile wangepata katika taifa la Karibea.

"Ninaamini kama nilivyosema, Wakenya wakija, kwanza kabisa watakuja kufanya mauaji katika jamii maskini kwa sababu viongozi na wanasiasa mafisadi watawaambia waende wapi kwa kisingizio kwamba wanakuja kuondoa magenge na majambazi, na wataingia katika jamii maskini kufanya mauaji, alisema.

Barbeque kwa sasa anaongoza kundi la G9 la magenge na kikundi cha wanamapinduzi cha Viv Ansanm (Kuishi Pamoja), muungano mpya wa magenge ulioanzishwa hivi karibuni. **KTN**

# KVZ FC YAANZA KUZIWINDA SIMBA, YANGA MUUNGANO

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya KVZ FC inaanza maandalizi yake kuelekea michuano ya Kombe la Muungano pamoja na michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), maarufu FA Cup, baada ya mapumziko mafupi katika kipindi hiki cha Mwezi wa Ramadhani.

Kwa mujibu wa ZFF, michuano ya Kombe la Muungano, itaanza kutimua vumbi Aprili 23, mwaka huu, kwa kushirikisha timu nne ambapo mbili kutoka Tanzania bara na mbili kutoka visiwani Zanzibar.

Kwa upande wa Zanzibar ni KVZ FC na KMKM SC wakati kwa kwa Tanzania Bara ni Klabu ya Simba na Yanga.

**Akizungumza na gazeti hili Kocha Mkuu wa timu ya KVZ, Ali Mohmed Ameir, alisema ana taka kupata wiki tatu za maandalizi kuele kea michuano hiyo ambayo ipo mbele yao kwa sasa.**

Alisema katika wiki hizi za mwisho wa mfungo wa Ramadhani, mpangilio wake ni kufanya mazoezi mara moja kwa siku na muda mzuri zaidi ni usiku wakati ambao tayari wachezaji wameshafungua.

Ameir alisema muda huo utakuwa rafiki ni mzuri kwa mwalimu kuweza kufanya mpangilio wake wa mazoezi kama alivyopanga kuliko asubuhi ambapo itamlazimu kufanya mazoezi mepesi tu.

"Kwa sasa tunamashindano matatu, kuna FA, Muungano lakini pia kuna Ligi Kuu Zanzibar, hivyo lazima tuwe na maandalizi ya nguvu ili tufanikiwe kufanya vizuri katika mashindano yote,"alisema.

Alisema mashindano ya Muungano yatakuwa na ushindani mkubwa kutokana na kuwapo kwa mchanganyiko wa klabu kutoka Bara na Visiwani, lakini pia uzoefu wa klabu hizo katika mashindano mbalimbali.

Hata hivyo, alisema mashindano yote yaliyo mbele yao anayapa uzito mkubwa na matamanio yake ni kuhakikisha anafanya vizuri kwa mashindano yote aliyoshiriki kwa msimu huu wa 2023/2024




Beki wa kushoto wa Simba, Mohamed Hussein 'Tshabalala', akimiliki mpira dhidi ya winga wa Al Ahly, Percy Tau, kwenye mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Ijumaa iliyopita na kumalizika kwa wageni hao kushinda bao 1-0, **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Moro Kids, Arusha City, vinara Ligi ya Mikoa nchini

**Na Adam Fungawamgo**

TIMU za Arusha City, Moro Kids ya Bokombe Kombaini, zinaongoza kwenye msimamo wa Ligi ya Mikoa hatua ya makundi inayoendelea kwenye vituo mbalimbali nchini.

Kwa mujibu wa msimamo uliotolewa na Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), Moro Kids inaongoza kwenye Kundi B linalocheza mechi zake kwenye Uwanja wa Tamco, Kibaha Pwani, ikiwa na pointi 12, baada ya kucheza mechi tano, ikishinda nne na kupoteza moja.

Timu hiyo inafuatiwa na Gunners FC ya Dodoma yenye pointi 11, na Stand FC ya Mtwara inayoshika nafasi ya tatu kwa pointi zake 10.

Arusha City ni kimara kwenye Kundi C, linalokipiga mechi zake Manyara, Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, ikiwa na pointi 13, ikicheza mechi sita, kushinda nne, sare moja na kupoteza moja.

Inafuatiwa na Eagle ya Dar es Salaam yenye pointi 12, Kawele FC ya Kilimanjaro yenye pointi 11 na ya nne ni Simiyu FC, ambayo ina pointi tisa.

Kundi D, linalokipiga Mwanza, Uwanja wa Nyamagana, linaongozwa na Bukombe Kombaini iliyojikusanyia pointi 14 kwa michezo sita iliyocheza, ikiwa imeshinda mechi nne na sare mbili.

Timu hiyo inafuatiwa na Leo Tena ya Kagera yenye pointi 13, Rock Solution ya Mwanza ambayo ina pointi 13 pia, na nafasi ya nne inashikiliwa na Friends Rangers ya Dar es Salaam ambayo ina pointi 10.

Kundi A, ambalo linacheza mechi zake Njombe halijacheza mechi zake kwa muda mrefu sasa, huku TFF ikiwa haijatoa sababu, lakini hadi mechi za kituo hicho zinasimama raundi ya tatu, Tukuyu Stars ilikuwa inaongoza ikiwa na pointi saba.

# Kachwele aendelea kuwika Canada

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Kimataifa wa Tanzania anayekipiga Klabu ya Vancouver Whitecaps inayoshiriki Ligi Kuu Canada, Cyprian Kachwele, ameendelea kung'ara baada ya kufunga kwenye michezo miwili mfululizo na kuisaidia timu yake kupata matokeo mazuri.

Vancouver Whitecaps ni Klabu ya Canada yenye makazi yake Vancouver. Pia hushindana kwenye Ligi Kuu Marekani (Major League Soccer- MLS), kama klabu mwanachama.

Kinda huyo aliyejiunga na timu hiyo akitokea Azam FC anakuwa mchezaji wa pili kutoka Tanzania kucheza ligi hiyo baada ya Nizar Khalfan aliyewahi naye kuichezea Vancouver Whitecaps.

Akizungumza na Nipashe jana, Kachwele, alisema amekuwa akiaminiwa na kupewa nafasi ya kucheza hali iliyomtengenezea kujiamini na kuendelea kufanya kazi yake vizuri.

Alisema anafurahi kuwa na mwendelezo mzuri na kiwango kinakuwa japo kuwa ni msimu wake wa kwanza kucheza ndani ya kikosi cha timu hiyo.

"Ni mazingira mapya kwangu, lakini taratibu naendelea kuimarika, ligi hii ni tofauti sana na nyumbani, mazingira yake ni mazuri lakini ina ushindani sana mchezaji unatakiwa kujitoa sana ili uweze kuisaidia timu ipate matokeo," alisema Kachwele.

Aliongeza suala la kutokata tamaa ni muhimu kwake kwani limemsaidia kupata nafasi katika kikosi cha kwanza na kutumia vizuri nafasi anayopewa.

Kachwele ni mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), aliyekuwapo Ivory Coast na hakutumika hata mchezo mmoja na ni miongoni mwa vijana waliotwa ili kupata uzoefu kwenye mashindano makubwa.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### VINICIUS HAWEZI KUHAMA

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, amesema hana wasiwasi kuhusu winga wa Brazil, Vinicius Jr, kuondoka katika klabu hiyo, baada ya uvumi kuwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, anaweza kuhama kwa sababu ya unyanyasaji wa kibaguzi. (***Diario Sport***)

### JAMES, GALLAGHER KUUZWA

CHELSEA inapanga kuwauza wachezaji wake wawili wa Kimataifa wa England - beki wa kulia, Reece James mwenye miaka 24, na kiungo wa kati Conor Gallagher mwenye miaka 24 - msimu huu ili kuepuka kukiuka kanuni za faida na uendelevu za Ligi ya Premia. (***Times***)

### TONEY KUTUA WEST HAM

KLABU ya West Ham inakaribia kumsajili mshambuliaji wa Brentford na England, Ivan Toney, mwenye umri wa miaka 28. (***Football Insider***)

### AMORIM KUBAKI LISBON

RUBEN Amorim amesema bado anataka Sporting Lisbon kushinda mataji huku kukiwa na tetesi kwamba anaweza kuchukua nafasi ya Jurgen Klopp kama kocha wa Liverpool. (***Star***)

### GREENWOOD NA UNITED

KOCHA wa Getafe, Jose Bordalas, amesema hajui mustakabali wa Mason Greenwood katika klabu hiyo, huku Manchester United wakiwa bado hawajafanya uamuzi iwapo mshambuliaji huyo wa England atarejea. (***Manchester Evening News***)

### GYOKERES BEI MILIONI 68

KLABU ya Sporting Lisbon inataka pauni milioni 68.5 kumnunua mshambuliaji wa Sweden, Viktor Gyokeres mwenye umri wa miaka 25, huku Arsenal na Chelsea zikimwania. (***Mirror on Sunday***)

### KIMMICH BASI TENA

KLABU ya Bayern Munich imethibitisha kuwa kiungo wa kati wa Ujerumani, Joshua Kimmich mwenye umri wa miaka 29, hataongeza mkataba wake katika klabu hiyo hadi watakapopata kocha mpya wa kuchukua nafasi ya Thomas Tuchel, ambaye anaondoka mwishoni mwa msimu huu. (Sky Germany, via 90min)

### BARCA, CHELSEA KWA WILLIAN

BARCELONA na Chelsea zote zinawania kumnunua Estevao Willian mwenye umri wa miaka 16 wa Palmeiras, huku kipengele cha kutolewa kwa winga huyo kikiripotiwa kuwa pauni milioni 51. (Mirror on Sunday)

### ERIKSEN ACHUKIZWA UNITED

KIUNGO wa kati wa Denmark, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 32, amechukizwa na kukosa muda wa kucheza Manchester United na ataruhusiwa kuondoka katika klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto. (Mirror on Sunday)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ENRIQUE NA NDOTO ZA MBAPPE KUBAKI PSG

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Paris Saint-Germain, Luis Enrique, amesema bado ana matumaini kwamba Kylian Mbappe anaweza "kubadili mawazo" na kubakia na klabu hiyo licha ya kuhusishwa na kuhamia Real Madrid katika majira ya joto.

**Vyanzo vilithibitisha kwa ESPN mnamo Februari kwamba Mbappe ameamua kujiunga na Madrid msimu wa majira ya joto baada ya mkataba wake na PSG kumalizika.**

Lakini wakati Madrid na Mbappe wapo kwenye mazungumzo, hakuna mpango wowote hadi sasa uliowekwa wazi.

●●● Siku zote nimekuwa na matumaini anaweza kubadilisha mawazo yake…

Kabla ya mechi yao dhidi ya mahasimu wao Marseille jana Jumapili, Enrique aliiambia Prime Video Sport France kwamba hajakata tamaa kuhusu wazo la mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ufaransa kubakia Paris.

Alipoulizwa kama ukweli kwamba itakuwa nafasi ya mwisho ya Mbappe kucheza Le Classique ungeathiri kikosi chake cha kwanza, Enrique alisema: "Kwa nini itakuwa dabi yake ya mwisho?

"Mimi, siku zote nimekuwa na matumaini kwamba Kylian anaweza kubadilisha mawazo yake - hajasema chochote kwa sasa. Anaweza kubadilisha mawazo yake.

"Fikiria ikiwa tutashinda mataji manne msimu huu na Kylian Mbappe ataamua dakika za mwisho kwamba anataka kubaki Paris.

"Kwa nini, tutaona."

"Kila kitu kinawezekana maishani. Ninachofahamu ni umuhimu kwa mashabiki wetu, kwa klabu na ushindani huu wa kihistoria."



# TUCHEL AKUBALI YAISHE BUNDESLIGA

**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA wa Bayern Munich, Thomas Tuchel amesema mbio za kuwania taji la Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, "ni wazi" zimekamilika baada ya timu yake kupoteza dhidi ya Borussia Dortmund Jumamosi na kua nyuma kwa pointi 13 dhidi ya vinara Bayer Leverkusen, huku zikiwa zimesalia mechi saba.

Dortmund iliishinda Bayern mabao 2-0 ugenini na kuwaacha Leverkusen ambayo haijafungwa kusubiri mechi tatu ili kushinda Bundesliga kwa mara ya kwanza.

Alipoulizwa kama mbio za ubingwa sasa zimekamilika, Tuchel, ambaye ataondoka mwishoni mwa msimu, aliiambia Sky Sport Germany: "Ni wazi, ndiyo.

"Baada ya mchezo wa leo (juzi), hakuna haja tena ya kuhesabu pointi sasa ni ngapi, hongera sana Leverkusen.

"Tumesikitishwa sana kwa sababu tulihisi hatukuleta shauku muhimu ya kushinda mchezo. Ilikuwa kidogo sana kutoka kwetu lilipokuja suala la msingi."

Karim Adeyemi na Julian Ryerson walifunga katika kila kipindi kwa ushindi wa kwanza wa ligi kwa Dortmund wakiwa Bayern ndani ya miaka 10.

Bayern, mabingwa mara 11, walibakia na uwezekano mkubwa wa kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya ili kuepuka msimu wao wa kwanza bila taji tangu mwaka 2012.

Bayern itacheza na Arsenal ugenini katika mkondo wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Aprili 9, mwaka huu.

Iwapo Leverkusen itafanikiwa kutwaa taji hilo, itakuwa ni mara ya kwanza tangu Dortmund kushinda mataji mfululizo mwaka 2011 na 2012 kwa timu nyingine isipokuwa Bayern.

# Ten Hag: Man United imeshindwa kupigana

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United walikosa "shauku" na "kupigana" katika sare ya bao 1-1 na Brentford, kwa mujibu wa kocha, Erik ten Hag.

United haikuwa kwenye kiwango katika Uwanja wa Gtech Community Jumamosi na wakabahatika kuchukua uongozi katika dakika ya 96.

Hata hivyo, Brentford walipata bao lililostahili kusawazisha kupitia kwa Kristoffer Ajer dakika ya 99 na baadaye Ten Hag alikiri kuwa timu yake haikuwa nzuri vya kutosha.

"Tulionesha uthabiti wakati wote wa mchezo, lakini Brentford walikuwa bora," alisema Ten Hag.

"Tunapaswa kuonesha shauku na hamu



zaidi katika nyakati nyingi kwenye mchezo. Lakini unaposhinda kuchelewa sana unapaswa kuleta juu ya mstari.

"Hatukucheza vizuri, lakini kulikuwa na roho, kulikuwa na vita, lakini haitoshi."

Matokeo hayo yaliharibu matumaini ya United kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, hasa baada ya Aston Villa na Tottenham - kukaa nafasi ya nne na ya tano kwenye msimamo - zote zilishinda mechi zao mapema siku hiyo.

"Bado kuna mechi nyingi za kuchezwa, lakini bila shaka pointi zitakuwa ghali zaidi mwishoni," alisema Ten Hag.

"Kulipaswa kuwa na tatu, lakini sasa ni moja tu na mwisho tutajua jinsi inaweza kufanya kazi, lakini inaweza kuwa hatua kubwa mwishoni."

United itacheza na Chelsea na Liverpool na licha ya Brentford kuwa na mashuti 31, Ten Hag alipuuza pendekezo la timu yake kuwa wazi sana nyuma.

United sasa wameruhusu mashuti 20 au zaidi katika mechi tisa kati ya 11 zilizopita.

"Nilielezea, tulilinda chini wakati mwingine na kwa sababu Brentford ni moja kwa moja tulipoteza mipira mingi ya sekunde na tulilazimika kulinda eneo la hatari," alisema Ten Hag.

"Tulikuwa na kipa mzuri (Andre Onana), alikuwa na kipaji usiku wa leo (juzi), lazima tuseme hivyo pia.

"Matokeo yetu ni thabiti kuanzia Januari na kuendelea. Tunaruhusu mikwaju, lakini haturuhusu mabao mengi."

# Pochettino alia na wachezaji Chelsea

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Mauricio Pochettino, amewashutumu wachezaji wake kwa kukosa njaa inayohitajika wakati timu yake ikilazimishwa sare ya mabao 2-2 nyumbani na Burnley iliyokuwa na wachezaji 10, Jumamosi.

Licha ya Cole Palmer kufunga mabao mawili, Burnley walitoka nyuma mara mbili na Dara O'Shea akasawazisha dakika za mwisho kwenye Uwanja wa Stamford Bridge.

Katikati ya msimu, Chelsea ilisalia katika nafasi ya 11, huku Burnley wakiwa nafasi ya 19.

"Leo (juzi), hatukuonesha uwezo, nguvu, njaa ambayo ni kiwango cha chini zaidi kushindana katika Ligi Kuu England," alisema Pochettino katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Katika safu ya ulinzi tuliruhusu mabao mengi sana ndiyo maana nimesikitishwa na kukatishwa tamaa.

"Ni zaidi juu ya kuwa na nguvu kama kikundi, kuwa na nguvu kuwa kama timu. Kwa sababu tofauti yetu tuko polepole sana katika eneo hili na hilo ndilo jambo kuu.

"Si kutafuta visingizio, lakini timu ilicheza vizuri, tulikuwa na nguvu tulipokuwa tunaenda mbele, lakini tulipokuwa hatuna mpira hatukuonesha nguvu sawa."

"Tumesikitishwa sana na kufadhaika kwa njia ambayo katika kipindi cha pili hatukushughulikia hali hiyo," alisema Pochettino.

"Sisi ni timu ambayo tunapocheza kumiliki mpira na kwenda mbele tuna uwezo wa kutengeneza nafasi nyingi, lakini hatukufunga kwa nafasi tulizotengeneza, tunatakiwa kuongeza asilimia ya mabao."

Palmer amekuwa mchezaji wa tano kufikisha mabao 20 katika msimu wake wa kwanza wa Ligi Kuu England akiwa na Chelsea.



## HABARI MICHEZO

## Gamondi: Dk. 90 zitaamua Sauzi

INATOKA UKURASA 24

tuliwaheshimu sana na kucheza mchezo wa kujihami na kukabiliana na mashambulizi ya kushtukiza (Counter attacks), licha ya kwamba tulikuwa uwanja wa nyumbani," alisema Gamondi.

Alisema hajababaika na umiliki wa mpira kuwa asilimia 30-70 kwa kuwa zilikuwa kwenye eneo la mpinzani wao kwani mipango ya mchezo ilikuwa ni kusubiri Mamelodi Sundowns katikati eneo ambalo wanalitumia kujenga mashambuliazi na wao wawashambulie kwa kasi na si kucheza nao kisa wapo nyumbani.

"Nawaamimi wachezaji wangu, Mzize (Clement) kijana na ana nafasi ya kuwa mchezaji mzuri wa Tanzania, si Yanga pekee na wachezaji wote wana nafasi sawa kikosini, umeona kazi aliyofanya tukiwa hatuna mpira kuzuia njia za pasi za Mamelodi Sundowns ?

"Kuwakosa Aucho (Khalid) Pacome (Zouzoua) ni pengo, lakini lazima tupongeze kazi ya Jonas Mkude ilikuwa bora, Aucho ni sehemu ya timu na Pacome pekee huwezi kushinda mchezo na 'tuliwamisi' hao wote na tulilazimika kuwatumia wachezaji waliopo kikosini," alisema Gamondi.

Aliongeza kuwa wana wachezaji 26, lakini pia wamemsahau Yao (Attohoula), na ana matumaini ya kuwatumia wachezaji hao kwenye mchezo wa marudiano Pretoria

"Matumaini yetu ni kufanya vizuri hata kufika fainali, michezo ya CAF si sawa na level nyingine ya mashindano yoyote na wachezaji tuliowakosa tumeziba pengo lao vem, naamini tunaweza kupambana kushinda Pretoria," alisema Gamondi

Naye Kocha wa Mamelodi Sundowns, Rhulani Mokwena, alisema walianza kipindi cha kwanza wakilenga kuwa na umiliki wa mchezo, lakini hawakuweza kufanya kwa ubora mkubwa.

"Tumepoteza mipambano mingi na mipira ya pili na kipindi cha pili tuliongeza ubora wa mchezo wetu, tumecheza dhidi ya timu nzuri na tulifahamu hautakuwa mchezo mzuri, lakini kwa matokeo haya tunafahamu tunapaswa kwenda kushinda Pretoria. "Yanga ni timu nzuri, tumezuia vizuri kwenye muda mwingi wa mchezo na kupambana dhidi ya Musonda (Kennedy), Mzize, Aziz Ki (Stephane), Max (Nzengeli), lakini tungeweza kutengeneza nafasi, pasi ya mwisho ndo kitu tulikosa, tutatazama kile tutakachoweza kufanya kwenye kipindi cha pili, tutakapokuwa nyumbani," alisema Mokwena.

Aliongeza kuwa awali kabla ya mchezo kwenye mkutanona wanahari alisema Yanga ni timu nzuri iliyofundishwa vema na walifahamu wanakutana na mchezo mgumu, na wamecheza kwenye joto kali, lakini wamefanya vizuri na wanatarajia kwenda kufanya vizuri zaidi nyumbani.

"Nitaenda kuzungumza na wachezaji juu ya ninavyosikia kuhusu mchezo huu, tunaweza kufanya vema zaidi tukiwa na mpira na hata kama tungeshinda ningesema hayo, tunapaswa kucheza vizuri zaidi kwenye mchezo wa pili," alisema Mokwena.

# PAMBA YAIPA MKONO POLISI, KENGOLD FC YAVUTWA SHATI

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuenguliwa nafasi ya pili kwa saa 24, timu ya Pamba FC juzi ilirejea kwenye nafasi hiyo kwa kuifumua Polisi Tanzania mabao 5-1, katika mechi iliyochezwa Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza, huku vinara wa ligi hiyo, KenGold wakibanwa mbavu kwa kulazimishwa sare ya 3-3 dhidi ya Mbuni FC.

Kabla ya mechi hiyo, Pamba iliteremshwa hadi nafasi ya tatu, baada ya Mbeya Kwanza kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Cosmopolitan na kukwea hadi nafasi ya pili ya msimamo wa Ligi ya Championship.

Ushindi huo wa mabao 5-1 umeirudisha tena kwenye nafasi ya pili ikifikisha pointi 58, ikibakisha mechi tatu tu za kumalizia msimu na kuisogeza Mbeya Kwanza nafasi ya tatu ikiwa na pointi 56.

Mabao ya washindi yalifungwa na Michael Samamba aliyefunga matatu, Issa Ngoa na Mashaka Adam.

Matokeo hayo yanaiweka kwenye nafasi nzuri Pamba kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao moja kwa moja kama itashinda mechi zake tatu zilizobaki.

Wakati hayo yakiendalea, vinara Kengold walishindwa kupata pointi tatu, wakilazimishwa sare ya mabao 3-3 ugenini, Uwanja wa Sheikh Abri Abeid jijini Arusha dhidi ya Mbuni FC.

Matokeo hayo yanaifanya timu hiyo kuendelea kuongoza ligi, lakini ikiwa na pointi 61, sasa ikihitaji pointi tano tu katika michezo mitatu iliyosalia ili kupanda Ligi Kuu.

Iwapo itazipata pointi hizo, itafikisha jumla ya pointi 66, ambazo ni Pamba tu ambayo inaweza kuzipita, huku Mbeya Kwanza kama ikishinda mechi zake tatu zilizobaki, itaishia pointi 65.

Kwingineko timu ya Mbeya City, ikiwa nyumbani, Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, ilipata kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya TMA katika mechi ya raundi ya 27 ya ligi hiyo ya Champioship ambayo ipo ukingoni.



# *Benchikha kazi moja na mastraika*

INATOKA UKURASA 24

ya kwanza kuzidiwa na ubora wa wachezaji wa wapinzani wao Al Ahly, anaimani na wachezaji wake kwenda kufanya vizuri kwa kufuata mbinu ambazo anawapa kuelekea mechi ya marudiano nchini Misri.

Alisema licha ya safu ya ushambuliaji kutokuwa na ubora, analazimika kuendelea kuwapa mbinu za kiufundi ili nchini Misri kupata matokeo chanya.

Kocha huyo alisema bado hawajakata tamaa kuelekea mchezo wa marudiano na anaamini kuwa wanauwezo wa kwenda kupambana ugenini na kufanikiwa malengo yao.

"Licha ya kuendelea kukinoa kikosi na kuwapa maelekezo juu ya mchezo wa marudiano, lakini kuna kazi kubwa naifanya ikiwamo kuzungumza na wachezaji wangu. Bado tuna nafasi ya kupata matokeo ugenini tukipambana zaidi," alisema Benchikha.

Alisema kuwa licha ya kutokuwa na ubora mkubwa, lakini ana matumaini makubwa ya vijana wake kwenda kupata matokeo mazuri ugenini kwa sababu ya kile anachoendelea kuwapa wachezaji wake kwenye uwanja wa mazoezi.

Benchikha alisema wamerudi katika uwanja wa mazoezi kufanyia kazi mapungufu yao na kuisuka vilivyo safu ya ushambuliaji ili kuhakikisha wanatumia vema nafasi zinazopatikana.

Aliongeza kuwa anaimani na kikosi chake katika mchezo wa ugenini kwa sababu waliwahi kucheza na Al Ahly nchini Misri na kutoka nao sare hali ambayo hata katika mechi ijayo wanaweza kupata matokeo mazuri.

Kikosi cha Simba leo kinaingia kambini kuendelea na mazoezi kwa ajili ya mchezo wa marudiano dhidi ya wenyeji wao Al Ahly, nchini Misri utakaochezwa April 5, mwaka huu.

Katika mchezo wa awali, Simba ilitengeneza nafasi saba zilizolenga lango, lakini ikashindwa kuzitumia huku Al Ahly nafasi yao moja tu waliyotengeneza wakiandaka bao hilo la mapema dakika ya sita lililodumu hadi mwisho wa mchezo.

# Michezo

Jumatatu Aprili 1, 2024

Nipashe






Enrique na ndoto za Mbappe UKURASA 21


MPAMBANO...




Winga wa Yanga, Augustine Okrah, akipambana kuwania mpira dhidi ya viungo wa Mamelodi Sundowns, Lucas Ribeiro Costa (kulia) na Marcelo Allende Bravo (kushoto), kwenye mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na kumalizika kwa sare tasa. **MPIGAPICHA WETU**

# Mashabiki wa Yanga SC wakerwa kiingilio bure

## ●●● Ni waliotoka mikoani wakiwa na tiketi na kuishia kuangalia mechi kwenye luninga Dar baada ya...

**Na Shufaa Lyimo**

BAADHI ya mashabiki wa Yanga kutoka mikoa mbalimbali nchini waliokuwa wamekuja jijini Dar es Salaam juzi kushuhudia mchezo wa robo fainali Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini wameulalamikia uongozi wa klabu hiyo kwa kitendo cha kuruhusu mashabiki kuingia uwanjani bure hali iliyozua tafrani kubwa na kuwanyima nafasi ya kuishuhudia mechi hiyo mubashara uwanjani.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na timu hizo kutoshana nguvu kwa sare tasa, uongozi uliruhusu mashabiki kuingia bure bila kulipa eneo lote la mzunguko ambalo ndilo linalochukua idadi kubwa zaidi ya watazamaji uwanjani hapo.

Kutokana na wingi wa mashabiki waliojitokeza na kila mmoja akitaka kuwahi nafasi, walivamia geti uwanjani hapo na kulivunja, hali iliyozua tafrani na wengine kuumia na kukimbizwa hospitali.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti baada ya mechi nje ya uwanja huo, baadhi mashabiki hao walisema kitendo hicho kimewasikitisha kwani wametumia gharama kubwa ya usafiri mpaka kufika Dar es Salaam, lakini wamelazimika kuangalia mchezo huo kwenye vibanda umiza na baa kutokana na kushindwa kuingia uwanjani.

**Walisema kwa hicho kilichotokea viongozi wa Yanga wanapaswa kujifunza na kubadilika kwani mchezo mkubwa kama huo hawakupaswa kuruhusu mashabiki kuingia bure.**

"Nimesikitika nimetoka Tunduma kuja hapa kuiangalia Yanga, nimekata tiketi mapema, lakini nimeambulia kuishia getini huu mchezo ni mkubwa ni bora wangeweka viingilio vya chini kila shabiki angelipa na kungekuwa na utaratibu mzuri kuliko hivi wanaweza kusababisha vifo vya watu wengi," alisema Kessy Hamisi.

Kessi alisema hajaridhishwa na uamuzi huo kutokana na gharama zake alizozitumia na kuwataka viongozi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), lifuatilie suala hilo vinginevyo ipo siku litaleta adhari kubwa.

Naye Zaituni Athumani kutoka Arusha, amewataka viongozi hao kutambua umuhimu wa timu kupata mapato kupitia mechi kubwa kama hiyo kwani nchi zilizoendelea huwezi kukuta kiingilio ni bure.

"Vya bure vinaua ndicho kitakachotokea, uwanja umezidiwa watu ni wengi mno binafsi nimelaani vikali kitendo hiki kwa kuwa malengo yangu hayajatimia, kwani sikuiona mechi," alisema Zaituni.

Karim Khamis kutoka Dodoma alisema: "Unapotanga mechi kubwa kama hii bure kwanza tunaishusha thamani klabu yetu na mashabiki watakuwa wakisubiri vya bure kila wakati, hii haipendezi wengeweka hata buku mbili, nimetoka Dodoma nimeishia kuangalia mpira baa, si bora ningebaki nyumbani.

"Kwanza ukisema bure tu hata vibaka wanaongezeka, wengi nimesikia wakilalamika kuibiwa, ustarabu unakuwa mdogo hata walinzi maalum wanazidiwa ndio maana hata geti likavunjwa, hii ni hatari."

Moses John kutoka Moshi, Kilimanjaro alisema: "Hii si haki, kabisa, yani nimeteketeza hela yangu kutoka Moshi hadi hapa kuja kuangalia mechi kwenye TV Dar es Salaam.

"Ifike wakati tujifunze kwa wenzetu Simba, ambao wao wanajisikia fahari kulipa kiingilio kwenda kuisapoti timu yao licha ya msimu huu kutokuwa na matokeo mazuri kama misimu iliyopita, lakini wao wanajaza uwanja kwa kukata tiketi, ni aibu kwetu mpaka tusikie ni bure."

Juma Jafari wa Dar es Salaam, alisema alifika uwanjani mapema lakini tayari watu walikuwa wameshajaa uwanjani na kulikuwa hakuna sehemu ya kupita kutokana na wingi wa watu.

## Gamondi: Dk. 90 zitaamua Sauzi

**Na Saada Akida**

BAADA ya suluhu katika robo fainali ya mkondo wa kwanza dhidi ya Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema hatua hiyo huamuliwa kwa dakika 180 na hizo ni 90 za kwanza, hivyo mechi bado ipo wazi kwa pande zote.

Amesema ana matumaini ya kwenda kupambana na kutumia vizuri dakika 90 zilizosalia katika mchezo wa marudiano dhidi ya Mamelodi Sundowns nchini Afrika Kusini na kufuzu kucheza nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Gamondi alisema anajivunia kiwango cha wachezaji wake kwenye mchezo wa juzi na kwamba walionyesha uwezo mkubwa kwa kupambana licha ya kushindwa kutumia nafasi zilizopatikana.

Alisema mchezo ulikuwa mgumu na ushindanai wa kimbinu baina ya timu nzuri na bora ya Mamelodi ambayo kwake ndiyo timu inayocheza mpira mzuri barani Afrika, hivyo anajivunia namna wachezaji wake wamecheza na kutengeneza nafasi nzuri zaidi za wazi.

"Mamelodi Sundowns wana ubora wa hali ya juu na uzoefu,


INAENDELEA UKURASA 23


## Benchikha kazi moja na mastraika

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha amesema anaendelea kukisuka kikosi chake hususan safu yake ya ushambuliaji kuelekea mechi ya mkondo wa pili ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly ya Misri.

Simba itarudiana na Al Ahly katika Uwanja wa Cairo, Misri Ijumaa wiki, ikiwa na mzigo mzito wa kupindua matokeo ya bao 1-0 baada ya kuadhibiwa Ijumaa iliyopita katika Dimba la Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Benchikha alisema licha ya mechi


INAENDELEA UKURASA 23



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >